Gazeti la kwanza la Kiislam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

JUZU 74 No. 172 | RABIU THANI 1434 AH | FEBRUARY 2013 | TABLIGH 1392 HS | BEI TSH. 500/=

Nukuu ya Qur'an Tukufu

Haimpasi Mwenyezi Mungu kuwaacha waaminio katika hali mliyo nayo mpaka Apambanue mbaya katika mwema; wala haimpasi Mwenyezi Mungu kuwajulisheni mambo ya ghaibu, bali Mwenyezi Mungu huchagua katika Mitume Wake Amtakaye. Basi Mwaminini Mwenyezi Mungu na Mitume Wake. Na kama mtaamini na mtaogopa, basi utakuwa kwenu ujira mkubwa. (3:180).

Ziara ya Khalifa Mtukufu Ulaya yaleta matumaini mapya

• *Hotuba zake zakonga nyoyo za wengi*

Na Jamil Mwanga
Dar es Salaam

Hadhrat Khalifatul Masih V a.t.b.a alitoa hotuba ya Ijumaa kutoka msikiti wa Baitul Futuh, London tarehe 21 Desemba, 2012. Katika hotuba hiyo alielezea kuhusu kumshukuru Mwenyezi Mungu na pia jinsi wageni mbalimbali mashuhuri na watu wengine waliohudhuria mkutano wakati alipokuwa akilihutubia Bunge la Ulaya. Huzur a.t.b.a alieleza jinsi watu hao walivyopokea kwa mwitikio chanya hotuba hiyo pamoja na matukio mengine mawili yaliyofanyika nchini Ujerumani.

Katika siku na zama hizi, ni Jumuiya Ahmadiyya pekee yenye heshima ya kusambaza ujumbe wa kweli wa Islam duniani kote. Tunatakiwa tumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwamba tumepata fursa hii adhimu katika jitihada zetu za kueneza ujumbe wa Masihi Aliyeahidiwa (amani iwe juu yake).

Hotuba ya Khalifa Mtukufu a.t.b.a kwa Bunge la Ulaya huko Brussels ilipokelewa kwa mikono miwili. Mkutano na waandishi wa habari pia ulifanyika ambapo tukio hilo liliripotiwa kwa wingi na vyombo vya habari.

Jamaat ya Uingereza ilichangia vyema maandalizi ya tukio hilo la kuhutubia Bunge la Ulaya ingawa waandaaji wakuu walikuwa baadhi ya wataalam wanaohusika na taratibu za Bunge la Ulaya. Tukio hili lilisaidia mno kuondoa dhana potofu zilizojengeka dhidi ya Islam.

Wakati wa ziara ya Khalifa Mtukufu a.t.b.a Ujerumani, tukio lilifanyika Hamburg kuadhimisha kupanuliwa kwa jengo la Jamaat ambalo liliongezwa kwa kujengwa minara. Watu wengi mashuhuri wa eneo hilo walihudhuria. Tukio lingine lilikuwa kuzinduliwa kwa jengo jipya la Jamaat Ujerumani ambalo pia lilihudhuriwa na watu wengi. Aidha, misikiti miwili ilizinduliwa ambapo wakati wa ufunguzi wa msikiti mmojawapo kati ya hiyo, majirani wanandoa wawili walifika kumpongeza Khalifa Mtukufu na kumpatia zawadi. Ilielezwa kuwa wakati ramani ya msikiti ilipokuwa ikiandaliwa, wanandoa hawa walikuwa wakipinga kwa kupiga kelele. Hata hivyo, kadiri siku zilivyokuwa zinaenda shaka yao iliondoka na wakati walipohudhuria sherehe za uzinduzi na kusikiliza hotuba ya Khalifa Mtukufu a.t.b.a nyoyo zao zililainika zaidi.



Hadhrat Mirza Masroor Ahmad a.t.ba, Kiongozi wa Jumuiya ya Waislam Waahmadiyya Duniani

Khalifa Mtukufu a.t.b.a alielezea jinsi baadhi ya wageni walivyovutiwa na hotuba yake alipokuwa akihutubia Bunge la Ulaya. Askofu mmoja aliyetokea Uswis alisema kwamba maneno ya hotuba

Habari kamili uk 3

Kwaheri Mpiganaji, karibu Mwanaharakati

Na Fadhili A. R. Mikilla -
Muhtamim T/Jadid, Majlis Khuddamul Ahmadiyya Tanzania

Katika kitabu maarufu cha hadithi za Mtume Muhammad (saw) kiitwacho SAHIHI MUSLIM katika mlango wa 'Imani" ipo kauli ya Mtume (saw) inayosema 'Tofauti kati ya mshirikina na Muislam ni Sala'. Ndio kusema kusingelikuwa na amri ya kusali basi tofauti kati ya makundi haya mawili ya watu isingalikuwepo, kauli kama hii naweza pia kuitumia katika hali ya mkanganyiko wa kimadhehebu miongoni mwa Waislam duniani kwa sasa. Kwa kusema Tofauti kati ya Jumuiyya ya Waislam wa Ahmadiyya na Waislam wengine ni "Uongozi". Naam ni nidhamu ya Uongozi ndiyo iliyoitoa Jumuiyya hii kutoka katika kijiji kidogo cha Qadian nchini India na kuifikisha katika nchi zaidi ya mia moja na tisini (190) duniani. Na ni kukosekena kwa Uongozi tu, ndiko kunako ufanya Umma wa Kiislam hivi leo kupoteza mwonekano chanya mbele ya uso wa dunia, kwani sote ni mashahidi wa jinsi Uislam unavyodhalilika na kupoteza nuru yake, sehemu mbalimbali duniani.

Ieleweke ya kuwa siyo lengo la makala haya kuelezea umuhimu wa kuwa na uongozi katika Umma wa Kiislam la! Bali madhumuni hasa yaliyonifanya mimi kushika kalamu na karatasi ni kwa ajili ya kumuaga

Endelea uk. 4

Imam wa Waislamu Atapatikanaje?

Bishara za ujaji wa kiongozi mkubwa wa kiroho zinapatikana katika vitabu vya dini zote takribani. Sawa na bishara hizo, kiongozi huyo, atadhihiri katika siku za mwisho wakati wa upotevu kupita kiasi. Kiongozi huyo ametajwa kwa majina tofauti. Waislamu waamini Nabii Issa (A.S.) ndiye yule kiongozi atakayerudi tena. Vilevile ni imani yao kwamba wakati huo huo atapatikana kiongozi mwingine ambaye anajulikana kwa jina la 'Imam Mahdi' (kiongozi anayeongozwa). Wakristo pia wanaitikadi kwamba Bw. Yesu Kristo atakuja mara ya pili. Ndiye kiongozi anayetabiriwa kuja. Na mabaniani wanamngoja Krishna. Masingasinga nao wana imani juu ya kuja wa kiongozi wao. Kabla ya kuendelea mbele, tungependa kutatua baadhi ya matatizo yazukayo kutokana na bishara hizi.

Sawa na bishara kuhusu ujaji wa kiongozi wa kiroho aliyeahidiwa, wakati wa kutokea kwake ni ule ule mmoja na alama za udhihirishaji pia ni za aina moja. Hivyo tatizo kubwa ni kwamba, je inawezekana yule kiongozi atokee katika kila dini yaani kila dini iwe na kiongozi wake? kama tukikubali wazo hili, dunia yetu hii itakuwa uwanja wa mapigano makali. Badala ya

Endelea uk. 2

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

Kutoka uk. 1

Imam wa Waislamu

kuwaunganisha. Wanadamu, viongozi hao watawatenganisha. Haiwezekani Mwenyezi Mungu apange mpango wa aina hii. Upande mwingine, bishara hizo ni za kweli kabisa, kwani hupatika katika vitabu vya dini zote. Kwa hakika, bishara hizo zote zilimhusu mtu mmoja tu, atakayekuwa na majina au sifa mbali mbali. Yaani, Mwenyezi Mungu atamwinua kiongozi mmoja tu ambaye atatimiza bishara zote zinazopatikana katika dini mbalimbali na kulingana na kazi zake mbali mbali atapewa majina mbali mbali.

Tatizo jingine ni kwamba huyo kiongozi anayengojewa, atakuwa mfuasi wa dini gani? jibu lake ni kwamba kiongozi huyo atatokea katika wafuasi wa dini iliyokamilika na inayodai ya kwamba imeletwa na Mwenyezi Mungu ili kuwaongoza wanadamu wote mpaka siku ya kiyama, nayo siyo nyingine ila ni dini ya kiislamu. Na katika mitume wote, ni Mtume Muhammad (s.a.w) pekee ambaye ametumwa kwa mataifa yote ya dunia nzima (Qur'an Tukufu 7:159). Hivyo, bila shaka mfuasi mmoja wa Mtume Muhammad (s.a.w) ndiye atakayepewa cheo cha yule kiongozi aliyetabiriwa.

Kwa mujibu wa imani ya baadhi ya waislamu viongozi wawili na vyeo tofauti, watatokea. Nabii Issa ndiye Masihi aliyeahidiwa naye atashuka kutoka mbinguni na Imam Mahdi atazaliwa katika Waislamu. Hivyo, sawa na imani yao hii, Masihi na Imam Mahdi ni watu wawili. Tumekwisha hakikisha juu ya kwamba haiwezekani watokee viongozi wengi wakati mmoja, kwani watasababisha mfarakano katika watu. Hivyo, sawa na kanuni hii, itatubidi kukubali kwamba atakayekuja ni mtu mmoja tu ila atapewa vyeo viwili. Na ndivyo alivyosema Mtume Mtukufu (s.a.w) kwamba: "LA MAHDIYYA ILA ISSA" (IBN MAJAH). Yaani mahdi siye ila Issa. Hadidhi nyingine iko wazi zaidi isemayo kwamba: "Ni karibu mtu yeyote atakayekuwa hai kati yenu akutane na Issa (a.s.) ameitwa Imam Mahdi pia. Hivyo, Masihi na Imam Mahdi si watu wawili, bali ni mtu mmoja mwenye vyeo viwili. Kwa sababu ya kuongozwa na Mwenyezi Mungu, anaitwa Mahdi na kwa sababu ya kuwaongoza wakristo pia, amepewa jina la Masihi.

Baadhi ya Waislamu wanaamini ya kwamba Masihi aliyeahidiwa ni yule yule wa zamani, aliyetumwa na Mwenyezi Mungu kwa wana wa Israeli. Lakini imani ya aina hii ni kinyume na mafundisho ya dini ya kiislamu. Sawa na Qur'an Tukufu na hadithi zilizo sahihi za Mtume Mtukufu (s.a.w.) Nabii Issa (a.s.) amekwisha fariki. Na sawa na Qur'an Tukufu wafu hawarudi duniani (23:101;39:48). Hivyo hamna swali la kurudi Masihi yule yule wa zamani. Tena, Mtume Mtukufu (s.a.w.) mwenyewe amesema kwa uwazi kabisa kwamba Masihi Aliyeahidiwa atatokea katika Waislamu. Hadithi yenyewe inapatikana katika kitabu mashuhuri kiitwacho "BUKHARI", ambayo tafsiri yake ni hivi " mtakuwaje atakapofika mwana wa Mariamu kazi yenu, naye atakuwa Imam wenu kutoka miongoni mwenu. Maneno ya Mtume (s.a.w.). "KUTOKA MIONGONI MWENU" yanahakikisha wazi kabisa kwamba Masihi Aliyeahidiwa, atatokana na waislamu, ambaye atazaliwa katika waislamu.

Tungependa kuwapasha habari njema wanadamu wote, Waislamu kwa Wakristo, Mabaniani kwa Masingasinga na wafuasi wa dini nyingine kwamba yule kiongozi aliyetazamiwa kufika, aliye kuwa akingojewa kwa hamu na kiherehere na mataifa yote, amekwishafika naye ni Seyyidina Ahmad (a.s.) Mwazilishi Mtakatifu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya. Ametumwa na Mwenyezi Mungu ili kuwaongoza watu wote kwenye dini ya kweli nayo ndiyo ISLAMU. Ni mwana wa kiroho wa Mtume Mtukufu Muhammad (s.a.w) aliyepata cheo cha unabii katika utii na ufanisi kamili wa Mtume Mteule Muhammad (s.a.w).

Seyyidna Ahmad A.S ambaye jina lake kamili ni Mirza Ghulam Ahmad, alizaliwa mnamo mwaka 1835 katika mji wa Qadian, India. Tangu ujana wake, alishungulikia sana ibada ya Mwenyezi Mungu na kusoma kitabu chake Kitakatifu yaani Qur'an Tukufu. Kwa kuwa Mwenyezi Mungu alimteuwa ili kumtumikia yeye na kumtumikia Mtume wake Mteule Muhammad (s.a.w.). Hivyo Seyyidna Ahmad (a.s) alitoa dhabihu ya kila aina kwa shabaha hizi. Alijitolea kiajabu kwa ajili ya dini ya Mwenyezi Mungu yaani ISLAM. Mwenyezi Mungu alimjalia elimu nyingi sana ya Kitabu chake, Qur'an Tukufu. Naye akatunga vitabu zaidi ya 80 ambavyo vimejaa maelezo na tafsiri ya Qur'an Tukufu. Alihakikisha kwa hoja madhubuti ukweli wa Qur'an Tukufu, ukweli wa Mtume Muhammad (s.aw.) na ubora wa dini ya kiislam na akawaita wapizani kuthibitisha ubora wa dini zao, lakini hakuna hata mmoja aliyejitokeza kwa mashindano haya. Alikuwa mpenzi ashiki wa Qur'an Tukufu. Akiisifu Qur'an Tukufu, Seyyidna Ahmad (a.s) anasema :Watu wengine huvutika na uzuri wa mwezi. Ama mimi mwezi wangu ni Qur'an Tukufu." Anaendelea kusema: "Daima natamani kuibusu Qur'an na kuizunguka kama mahaji wanavyoizunguka Ka'ba. Mimi Ka'ba yangu ni Qur'an".

Seyyidna Ahmad aliaga dunia mnamo mwaka 1908 na baada ya kufariki kwake desturi ya Ukharifa ilianza ambayo kwa rehema ya Mwenyezi Mungu inaendelea katika Jumuiya. Tunamwomba Mwenyezi Mungu audumishe Ukharifa mpaka siku ya kiyama.

Ziara ya Khalifa Mtukufu Ulaya

Kutoka uk. 1

hiyo yalikuwa yana mvuto wa kipekee. Huku yakitamkwa kwa ulaini, maneno hayo yalikuwa na utukufu na nguvu za aina yake. Alisema kuwa hajawahi kumwona mtu jasiri kama Hadhrat Khalifatul Masih. Mwislam mmoja kutoka Bunge la Ubelgiji alisema kwamba hotuba hiyo ya Khalifa Mtukufu a.t.b.a ilikuwa ni jambo la kujivunia kwa waislam wote na aliongeza kwamba imewapandisha daraja. Mwakilishi kutoka Wizara ya Mambo ya Ndani ya Ubelgiji alisema hotuba hiyo ilimhamasisha na kumsisismua kila mmoja. Mbunge mwingine wa Bunge la Ulaya, Godfrey Bloom alisema kwamba hotuba ya Khalifa Mtukufu a.t.b.a ilitoa nuru kwa kila mtu. Naye, mwakilishi kutoka Serikali ya Ufaransa Bw. Eric alisema kwamba hotuba hiyo ilikuwa yenye mwongozo wa kutosha kwa Ufaransa. Kwa upande wake, mtaalam kutoka Bunge la Uhispania alisema kwamba anaunga mkono barabara hoja zilizobainishwa kwenye hotuba hiyo. Mjumbe mwingine kutoka Uhispania alisema kwamba kwa mujibu wa Khalifa Mtukufu a.t.b.a umuhimu wa dini ni kuongeza mapenzi miongoni mwa watu. Bw. Santiago, Profesa wa Sheria wa Chuo Kikuu ambaye amewahi kuandika vitabu kadhaa kuhusu Islam alimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kukutana na kila mmoja kwenye tukio lile. Alisema kwamba ingawa yeye ni mtu wa kiroho lakini kwa muda mrefu sana hajawahi kuona mandhari ya kiroho kama aliyoiona wakati Khalifa Mtukufu a.t.b.a alipokuwa analihutubia Bunge la Ulaya. Mama mmoja ambaye ni Mwanasheria kutoka Uhispania alisema kwamba alielezwa na mwenyeji wake muahmadiyya kwamba uzoefu atakaoupata hautokuwa na kifani, ukweli ambao ulithibitika. Alisema kwamba jitihada zinazofanywa na Jumuiya Ahmadiyya kwa hakika zitazaa matunda.

Wakati huo huo, Profesa kutoka nchini Malta alisema kwamba maandalizi ya tukio hilo yalikuwa mazuri sana. Alisema hotuba ya Khalifa Mtukufu a.t.b.a iliashiria amani ya dunia. Kwa upande wake, mtayarishaji wa vipindi vya televisheni kutoka Malta ambaye aliifahamu Jumuiya ya Ahmadiyya kwa kupitia mpango wa sasa wa usambazaji wa vipeperushi alisema kwamba kazi zinazofanywa na Jamaat Ahmadiyya katika kujenga amani ni za kuthaminiwa sana na kwamba baada ya kuonana na Khalifatul Masih a.t.b.a alibaini kuwa jambo hilo lilikuwa limezidi matarajio yote ukilinganisha na vile alivyokuwa akimsikia hapo kabla.

Mjumbe kutoka kanisa moja la Ulaya alisema kwamba Khalifa Mtukufu a.t.b.a alimpa kila mmoja ujumbe wa kuufanyia kazi kuhusu amani. Naibu Meya kutoka Ufaransa alisema hotuba ya Hadhrat Khalifatul Masih a.t.b.a ilikuwa nzuri sana. Profesa wa chuo Kikuu kutoka Ufaransa alisema kwamba alijiona mwenye bahati kubwa kuhudhuria tukio hilo chini ya uongozi wa Hadhrat Khalifatul Masih na alimtaja kuwa ni mdau wa kweli wa amani.

Charles Tannock, Mbunge wa Bunge la Ulaya, alisema kwamba Jumuiya ya Waislam Ahmadiyya inahubiri ujumbe wa amani katika kiwango cha dunia. Alisema kuwa amevutiwa zaidi na kipindi cha maswali na majibu wakati wa mkutano na waandishi wa habari. Alizungumzia kuhusu maendeleo ya Jumuiya Ahmadiyya na kusema kwamba watu wachache sana walikuwa wanafahamu kuhusu mafundisho yao na kwamba Bunge la Ulaya linawajibika kusambaza mafundisho haya kote barani Ulaya. Alisema Jumuiya Ahmadiyya ni mfano mzuri sana wa kudumisha amani na kuvumiliana. Alimshukuru Hadhrat Khalifatul Masih kwa hotuba yake iliyovuta hisia ambayo alisema kuwa ndio mafundisho ya kweli ya Islam. Aidha, alitaja majukumu yaliyopaswa kutekelezwa na nchi za Magharibi na zile za Umoja wa Ulaya. Alisema alistajaabishwa na ujasiri wa Hadhrat Khalifatul Masih a.t.b.a katika hotuba yake jinsi alivyoelezea suala la uhamiaji.

Mjumbe kutoka Estonia alisema kwamba Jumuiya ya Waislam Ahmadiyya inapinga masuala ya siasa kali. Aidha, alisifu kile alichokiita kuwa ni itikadi njema na ya kivitendo ya kukusanyika na watu wa dini mbalimbali. Mbunge mwingine wa Bunge la Ulaya alisema kwamba kitendo cha Hadhrat Khalifatul Masih a.t.b.a kuwepo mjini Brussels kuhutubia Bunge la Ulaya kinaonyesha kwamba watu wanataka kufahamu zaidi kuhusu Islam. Mbunge mmoja kutoka Ujerumani alisema kwamba Hadhrat Khalifatul Masih amehutubia Bunge la Uingereza na pia alitoa hotuba kule Capitol Hill, na kuongeza kwamba sasa atajaribu kufanya mpango ili Huzur a.t.b.a aweze kuhutubia Bunge huko Berlin.

Kuhusiana na tukio la Hamburg lililofanyika siku iliyofuata, ambalo nalo lilivutia, afisa mmoja alikaririwa akisema kwamba Khalifa Mtukufu a.t.b.a ameeleza vizuri sana mafundisho ya Islam na baada ya kumsikiliza ameweza kufahamu mafundisho halisi ya Islam. Mjumbe wa Baraza kutoka Hamburg alisema kwamba jinsi Hadhrat Khalifatul Masih a.t.b.a alivyokuwa akitamka maneno yake yaliathiri nyoyo kweli kweli. Alisema jinsi dhana ya Islam ilivyowasilishwa aliiona ni mpya kabisa. Wengine walisema kwamba shaka yao imeondoka baada ya kubaini mafundisho ya Islam kuhusu amani. Ilielezwa kwamba haiba ya Hadhrat Khalifatul Masih a.t.b.a inaonekana mithili ya mfalme aliyezungukwa na wanajumuiya wanaofanya kazi na kujitolea sana kwake. Waandishi wa habari pia walikuwepo ambao awali waliokuja kufanya mahojiano na Amir Sahib wa Ujerumani lakini waliamua kuwa na kipindi cha maswali na majibu na Hadhrat Khalifatul Masih. Hata hivyo, baada ya kusikiliza hotuba yake walisema kuwa madukuduku na maswali yao yote yameshajibiwa. Mama mmoja kutoka Kamati ya Bodi ya Islam pia alihudhuria. Mama huyu ambaye amezoea kuwa kimya dhidi ya Jamaat yetu lakini sasa amebadilisha mtazamo. Mama huyu alisema kwamba shaka yake yote imetoweka na pindi alipomwona Hadhrat Khalifatul Masih a.t.b.a alihisi kuwa ni aina ya kiongozi ambaye siku zote amekuwa akifikiri kuwa waislam wanamhitaji. Rais wa Polisi wa mjini Hamburg pia alikuwepo ambaye alisema kwamba kama mafundisho yaliyoelezwa kwenye hotuba yangalitekelezwa basi hakungekuwa na haja ya kuwepo polisi kama yeye. Tukio hili liliripotiwa vyema na magazeti yaliyoenea sehemu kubwa.

Maoni yaliyopokelewa wakati wa uzinduzi wa jengo la Jumuiya yalisema kwamba hotuba ya Hadhrat Khalifatul Masih a.t.b.a haikuwa hotuba bali ilikuwa ni sauti ya moyo wake na kwamba pamoja na kuwa ya kidini mwonekano wake ni wa kimatendo zaidi. Maoni mengine yalikuwa kwamba hotuba ilikuwa mashuhuri sana na maneno yanayogusa maisha hayajikiti tu katika mafundisho mema bali yameacha mvuto mkubwa kwa wasikilizaji.

Mwenyezi Mungu Ajaalie matukio haya yote yazidi kuleta matokeo na athari njema ya kudumu na Atuzidishie Taqwa na shukrani, Amin.

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Mahmood Hamsin Mubiru.
Kompyuta: Abdurahman M. Ame.
Mchapishaji: Sheikh Muhammad Arif
Msambazaji: Mwl. Omar Mnungu
Wajumbe: 1. Abdullah Khamis Mbanga
2. Swaleh Kitabu Pazi
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu@yahoo.com

Kwaheri Mpiganaji, karibu Mwanaharakati

Kutoka uk. 1

Kiongozi wa Khudam (Vijana) wa Jumuiyya ya Waislam wa Ahmadiyya aliyemaliza muda wake ndugu Alli Hamisi Mbambwa na kumkaribisha Kiongozi mpya Dr. Swaleh Kitabu Pazi, ambaye hivi karibuni amechaguliwa na Majlis Shura ya Khudamul Ahmadiyya hapa nchini, na kuthibitishwa na Hadhrat Khalifatul Masih V (atba) kuwa "SADR" mpya wa Majlis Khuddam (yaani Raisi wa vijana).



Sadr Khuddam aliyemaliza muda wake Ally Khamis Mbambwa (katikati) akiwa mbele ya jukwaa pamoja na Sadr Khuddam wa sasa Dr. Swaleh Kitabu Pazi (aliyesimama) wakati wa Ijtimaa ya Khuddamul Ahmadiyya 2012. Kushoto ni Amir na Mbashiri Mkuu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiya Tanzania Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry

Katika ziara iliyofanywa na Hadhrat Khalifatul Masih V (atba), mnamo mwezi wa May mwaka 2005 hapa nchini, Khuddamul Ahmadiyya wakati huo waliwahi kumuuliza Huzur, kwamba anawaonaje Khuddam wa Tanzania? Khalifatul Masih aliwajibu kwa kusema "Kwa nje mnaonekana mpo vizuri (strong), lakini kwa ndani inawapasa mfanye bidii kubwa ya kujitambua ili muwe na sura ya kuwa uti wa mgongo wa Jamaat". Kuondoka kwa Huzur kulifuatiwa na uteuzi wa Mheshimiwa Alli Saidi Mosse ambaye kwa hakika amefanya makubwa katika uongozi wake, na sote ni mashahidi juu ya hili, ila niseme jambo moja, kama kuna kitu ambacho historia ya Jamaat hapa nchini haitoacha kumtaja Amir huyu, basi ni uteuzi wake kwa ndugu Alli Hamisi Mbambwa Sahib kuwa Kaimu sadr wa Majlis Khuddamul Ahmadiyya hapa nchini. Naam alikaimu nafasi iliyokuwa ikishikiliwa na Al-akhi Abdullah Hamisi Mbanga (ambaye katika tasnia ya ushairi anaitwa Kungwi) aliyehamia Kibiti wakati huo kwa harakati za kimaisha.

Ni agizo la Qur'an Tukufu alilokuwa akilitimiza la 'Fantashiru fil ardhi' -yaani tawanyikeni katika ardhi (kwa kutafuta fadhili za Mwenyezi Mungu).

Uteuzi huo, kwa hakika ulikuwa tiba mujarabu iliyotosha kumtibu "Mgonjwa Khuddam" aliyekuwa anaumwa wakati ule, kurasa chache za makala hii hazitoshi asilani kuyaeleza aliyoyafanya Kaimu Sadr huyu ila itoshe tu kusema "Mwenye macho haambiwi tazama", kwani Bwana huyu licha ya kuwa rafiki yangu wa karibu sana, ninamfahamu Alli Hamisi mtoto wa Kainuza kama mpiganaji tena wa njia zote za dini na dunia, lakini mara baada ya kukabidhiwa amana hii ya uongozi ndugu huyu harakati za kidunia ni kama aliziweka kando, na mbele yake kulikuwa na kazi moja tu ya kuhakikisha Majlis Khuddamul Ahmadiyya Tanzania inasimama vilivyo.

Sisi sote bila shaka tutakuwa ni mashahidi, mpiganaji huyu alihakikisha Tanzimu ya Khuddam hapa nchini inajitambua na kuwa na muundo unaoeleweka, naam, hivyo ndivyo ilivyokuwa. Leo Khuddam tunajua kiapo chetu, leo Khuddam tunayo Ofisi yetu, tunayo katiba yetu, na zaidi ya yote tunajua wajibu wetu. Kwa upande wangu niseme tu, kama si nidhamu za kikatiba za jamaat, basi Bwana huyu ilitakiwa kifo tu ndio kitutenganishe na sio umri, lakini jambo kubwa tunaishi chini ya nidhamu, na utii, na kwa ujumla tunamtakia kila la kheri huko aendako kwenye Tanziim ya Ansarullah. Tunaamini kwa aina ya uchapakazi wake uliotukuka nao watafaidika nae na bila shaka watakuwa wameokota pochi ya fedha katikati ya maandamano, kwani mazuri aliyofanya katika Tanzimu ya Khuddam naamini yatakuwa chachu ya mafanikio kwa Ansarullah pia.

Si lengo langu, na kamwe sina nia ya kumfanyia kampeni akawe SADR na huko, bali kwa Alli ninayemfahamu hata kabla ya kuwa Sadr Majlis Khuddam kwa hakika utendaji wake katika masa'ala ya Jamaat si wa kutilia shaka, na daima hupenda kuona jambo la Jumuiyya linakwenda mbele na hujitoa mhanga hasa ili jambo lolote la Jamaat lifikie malengo yake. Niliishi naye katika Jamaat ya Mtibwa kipindi ambacho hakukuwa na Mwalimu yeyote wa Jamaat, lakini mambo yote ya Jamaat ya Mtibwa yalisimamiwa naye, huku yeye akiishi kule kama muhamiaji aliyekwenda kutafuta maisha. Kwa mukhtasari sisi kama vijana hatuna cha kukulipa ila Allah Ndiye Anayejua Akulipe nini. Kwani aliwahi kuulizwa Mzee Alli Saidi Mosse akiwa Amir wakati ule, miezi michache tu baada ya kumteua ndugu Mbambwa akaimu nafasi ya sadr kwamba anaionaje Khuddam chini ya uongozi wa Bw. Alli Hamisi Mbambwa? Yeye akasema hali yao kwa sasa "Ni sawa na maiti kutembea". Sasa ndugu zanguni mtu ambaye ameweza kufufua watu waliokuwa kama wafu, na wakaanza kutembea, tunaweza kumlipa chochote? Zaidi ya kumwombea kwa Mwenyezi Mungu? Mimi nadhani hatuwezi kumlipa, kama ilivyo kwa mzazi yoyote hakuna mtoto anayeweza kudiriki kumlipa mzazi wake chochote ambacho kitalingana na thamani ya malezi aliyolelewa mtoto husika.

Hivyo mimi nawaomba ninyi msomao makala haya tuungane nami katika maombi kwamba Mwenyezi Mungu Azipokee juhudi zake ndugu Mbambwa kijana wa marehemu mzee wetu Kainuza mzaliwa wa Kigoma. Pia niseme jambo moja ya kuwa bado Tanzimu ya Khuddam itaendelea kuhitaji msaada wake japo wa mawazo, ushauri n.k, kwani aliupigania vilivyo uhai na uzima wa Tanzimu ya Khuddam iliyokuwa inaelekea kusiko julikana. Wengi wetu ni mashahidi wa hali ya Khuddam ilivyokuwa hapo nyuma, bila shaka lilibaki jina tu, la Majlis Khuddam, lakini leo kwa msaada wa Allah na kwa juhudi zake binafsi, ukiizungumzia Majlis Khuddamul Ahmadiyya Tanzania basi hata nchi jirani za Kenya na Uganda wanaisikia sauti hiyo. Hii ina maana moja kubwa, kama tukiyaenzi yale aliyotuachia basi tutarajie Khuddam yenye ufaulu mkubwa na ambayo itakuwa mfano wa kuigwa miongoni mwa Majlis nyingi za Khuddam barani Afrika hata duniani kwa ujumla.

Mwisho niseme tu, KWAHERI MPIGANAJI, ULOFANYA KILA LILILOBUDI, ILI MAJLIS KHUDDAM IPATE UHAI. Naam sasa hivi si Khuddam pekee wanaojivunia Ukhuddam wao, bali hata makundi mbalimbali ya kijamii nje ya Jamaat, ukitaka kuthibitisha hilo nenda Kindwitwi ile kambi ya wenye matatizo ya ugonjwa wa Ukoma, nenda hospitali za Amama, Temeke na Mwananyamala, nasi huko tu bali fika pale Msimbazi Centre kisha uliza kituo cha taifa cha 'Damu salama' ukifika hapo ulizia kama wanaifahamu Majlis Khuddamul Ahmadiyya na Jamaat kwa ujumla, bila shaka utapewa maelezo mengi ya jinsi Tanzimu hii na Jamaat kwa ujumla ilivyokuwa mstari wa mbele na mfano wa kuigwa katika kuihudumia Jamii bila kujali dini, rangi, kabila n.k, naam maana ya Khuddam ni wahudumu. Kwa neno zima mambo haya mengi kama si yote yalifanywa chini ya uongozi wake, ambaye mimi bado sisiti kumuita "Mpiganaji" tena mwenye cheo cha "Kamanda".

Mungu ibariki Tanzania, ibariki Majlis Khuddamul Ahmadiyya lakini pia Mbariki Alli Hamisi Mbambwa na familia yake, na Umpokelee juhudi zake, katika kila hatua ya maisha yake. Amin Yaa Rabbil A'alamiin.

MJUE SADR MPYA WA MAJLIS KHUDDAMUL AHMADIYYA TANZANIA

Wazaramo wanao msemo mmoja unaosema "Ding'oka hingo! Dibwela hingo! Yaani ni sawa na kusema ameondoka "Kaisari" amefika "Kaisari".

Katika kikao cha "Shura" ya Khuddam kilichofanyika mnamo mwezi wa Oktoba mwaka 2012, Majlis Khuddam kwa ruhusa na baraka za Khalifatul Masih V (atba) ilifanya uchaguzi wa kumtafuta kiongozi mpya wa vijana (Khuddam) hapa nchini, (baada ya yule aliyekuwa akishikilia nafasi hiyo kumaliza muda wake kwa misingi ya umri) ambapo kiognozi huyo kwa lugha ya kiitifaki anaitwa SADR (Raisi). Majina kadhaa yenye sifa stahiki yalipendekezwa na mapendekezo hayo yalipigiwa kura na hatimae kupelekwa Markaz kwa Huzur (atba) kwa uthibitisho rasmi na mwisho wa yote jina la SWALEH KITABU PAZI, lilithibitishwa na hivyo kuvikwa rasmi joho la kuwa SADR.

Majlis Khuddamul Ahmadiyya Tanzania kwa kipindi cha miaka miwili ijayo, Swaleh Kitabu Pazi ambaye kitaaluma ni Daktari, na ni muajiriwa wa serikali katika hospitali ya taifa ya Muhimbili, alizaliwa miaka 36 iliyopita, jijini Dar es salaam. Yeye ni Ahmadiyya kwa kuzaliwa, na kama utachunguza kwa makini jina la mwisho katika majina yake matatu utagundua kuwa ni Mzaramo kwa kabila, kwani sikuwahi kumsikia 'Pazi' Mmakonde, Msukuma au Mngoni. Tusomao historia tunajua Pazi Mazongera alikuwa chifu wa wazaramo, na ni moja ya koo kubwa katika makoo ya kizaramo.

Bwana huyu kabla ya kuchaguliwa kuwa Sadr mpya wa Majlis Khuddam alikuwa na cheo cha Mu'utamad yaani Katibu wa Sadr aliyemaliza muda wake. Katika nafasi hiyo alionyesha utendaji uliotukuka, kwani alikuwa kiungo muhimu sana kati ya Sadr na wajumbe wengine wa Majlis. Kila alichotakiwa kukifanya sawa na maelekezo aliyopewa na Sadr alikifanya kwa kiwango cha juu. Tuliopata bahati ya kuwa wajumbe wa Majlis Khuddam pamoja nae yeye akiwa Katibu, tunajua utendaji wake ulikuwa ni wa aina gani? Kwani pamoja na kukabiliwa na masomo ya Udaktari (wale wasomi wanajua ugumu uliopo wa masomo haya), lakini alijitahidi vilivyo kutimiza wajibu wake katika Mas'ala ya Jamaat pia. Kwani aliweza kusafiri na sadr katika ziara ndefu za mikoani na kuyakabili majukumu yake ipasavyo. Niwashauri ndugu zangu wale wasomi wa fani mbalimbali kama Uhandisi, Uhasibu, Sheria, n.k ambao ni Khuddam na Wanajamaat kwa ujumla basi wajitahidi kuiga mfano wa "Kioo hiki" kwanza mimi sioni tofauti kati ya Sadr aliyepita na huyu mpya tuliyenae ni umri tu kwani kama kuna mtu aliyekuwa karibu sana kwa kila dakika ya utendaji wa Sadr aliyepita, basi ni huyu Dr. Swaleh Kitabu Pazi na kwa hakika anayo mengi ya kujifunza kutoka kwa Sadr aliyemtangulia, na anastahili hasa kurithi mikoba yake.

Na siku zote waswahili husema 'Anayerithi huzidi' lakini pia ni fundisho la Qur'an Tukufu pale Allah Anaposema "Wakati ujao ni bora kuliko uliopita. Basi nasi hatuna budi kutarajia yaliyo bora zaidi Inshallah. Lakini kwa sharti moja kubwa la kumwamini na kumsaidia. Bila shaka tutaweza hilo kama kila mmoja wetu atatimiza wajibu wake, kuanzia viongozi mpaka Khuddam wa kawaida. Nisema tu ya kwamba ule ushirikiano tuliouonyesha kwa Sadr aliyemaliza muda wake, basi na tuuonyeshe maradufu kwa Sadr huyu mpya na wajumbe wake wote. Bado naona mwanga mbele wa mafanikio makubwa wa Majlis Khuddam mpya chini ya Sadr huyu. Mwisho niseme tu KWAHERI 'MPIGANAJI' ALLI HAMISI MBAMBWA SAHIB, KARIBU 'MWANAHARAKATI' DR. SWALEH KITABU PAZI SAHIB.

Wa akhir Dawana Anil hamdulillah Rabbil A'alamin

Umuhimu wa Elimu katika Islam

Hotuba iliyotolewa na Sheikh Asif Butt katika Jalsa salana 2012.

Inaendele kutoka toleo lililopita

Kuhusiana na kujifunza elimu utotoni, Sayedena Ahmad a.s. anasema "*dini uluum ki tehsiil ke lie tafuuliat ka zamana buhat hi munasib aur mauzun he. Jab dari nikal aae, tab zarab, yazrebo, yaad karne bethe to kya khak ho ga, tafuliat ka hafiza tez hota he, insani umar ke kisi dosre hise men aesa hafiza kabi bi nahi hota, muje khuub yaad he ke tafuuliat ki baadh baaten ab tak yaad hen lekan pandra baras pehle ki aksar baten yaad nahin*" "yaani wakati wa utotoni ndio wakati mzuri na wenye kufaa sana kwa ajili ya kujifundisha elimu za kidini. Na baada ya kuota ndevu , mtu akianza kujifunza zarab, yazrebo, atashindwa. Ubongo wa utotoni huwa ni mkali sana na ubongo mkali wa namna hii haupatikani katika sehemu nyigine yo yote ya maisha. Najua vizuri sana kwamba baadhi ya mambo ya utotoni nayakumbuka mpaka leo lakini sikumbuki mambo mengi yaliyotokea miaka kumi na mitano iliyopita.

Tena katika hadithi moja Mtume s.a.w alisema " tafuteni elimu kwa juhudi kubwa kuanzia utotoni hadi uzeeni ." hapo mkazo mwingi umetiwa juu ya kuitafuta na kuipata elimu bila kuanglia mpishano wa umri. Hazrat Mirza Masroor Ahmad a.t.b.a khalifa mtukufu wa Masihil Mauud a.s ,safari moja akiwahutubia watoto alisema " kila mtoto wa kiahmadiyya anayo haki ya kujifunza elimu , na mtoto ye yote asiache masomo yake kwa sababu ya matatizo ya kifedha , kama mali ndiyo kikwazo katika kuitafuta elimu , basi niambieni mimi , insha allah mtasaidiwa kifedha , ni lazima kujifunza elimu hata kama mkabiliane na matatizo mengi". Tena Mtume s.a.w akieleza umuhimu wa kujifunza elimu , alisema " jifunzeni elimu hata kama mkalazimike kwenda china kuipata". Kisha akibainisha ubora wa kuitafuta elimu , alisema " atembeaye njia akitaka kujitafutia elimu humo , Mwenyezi Mungu atamrahisishia njia ya kwenda peponi. Na malaika humtandazia mtafutaji elimu mabawa yao kwa kumfurahia ayatendayo. Na wote waliomo mbinguni na ardhini hata samaki wa majini humwombea ghofira mtaalamu. Na ubora wa mtaalamu juu ya mwenye ibada ni kama ubora wa mwezi juu ya nyota nyinginezo. Maulamaa ndio warithi wa manabii." Hali kadhalika safari moja , mbele ya Mtume s.a.w walitajwa watu wawili , mmoja akiwa mwenye ibada na mwingine mtaalamu. Basi Mjumbe wa Allah s.a.w alisema : mtaalamu ni bora kuliko mwenye ibada jinsi nilivyo bora kuliko mtu ye yote wa kawaida kati yenu." Na ndani ya Qur'an Tukufu Mwenyezi Mungu anatoboa " *innama yakhshall Allaha min ibaadehil ulamaao"* yaani wenye kumwogopa kweli kweli Mwenyezi Mungu miongoni mwa watumishi wake ni maulamaa tu.

Ndugu wasikilizaji ,msingi wa dini ya haki ni elimu ya kweli iliyotoka kwa Allah ambayo haina budi kupatikana kwa vyo vyote vile. Jinsi alivyoagiza Mtume s.a.w , wazazi lazima wawafundishe watoto wao elimu ya dini kuanzia utotoni na hii ni njia moja bora ya kuwalea watoto vizuri. Malezi ya watoto huhitaji bidii kubwa na juhudi za mfululizo , watoto wanahitaji kupewa maelezo kila wakati . pengine wazazi wanaweza kukosea katika kazi hii , kwa hiyo kutokana na udhaifu wa kibindamu , kuwafanyia maombi watoto ni jambo muhimu sana isije udhaifu huo ukawa ni kikwazo katika malezi ya watoto. Maombi ya wazazi kwa ajili ya watoto wao, hupata kubuli mbele ya Mwenyezi Mungu. Mtume s.a.w alisema " maombi ya aina tatu hukubaliwa sana na Mwenyezi Mungu (1) maombi ya wazazi kwa ajili ya watoto wao (2) maombi ya msafiri (3) maombi ya mtu aliyedhulumiwa. Na katika hadithi nyingine Mtume s.a.w alisema " *duaul walede lewaladehikadua innabiyye le ummtehii."* Yaani dua ya baba kwa ajili ya mwanae ni sawasawa kabisa na dua ya nabii kwa ajili ya ummati wake. Kwa hakika kazi ya malezi ni jambo muhimu sana , kasoro za wazazi zinazojitokeza katika malezi zinakamilishwa kwa kumwomba na kumwelekea Mlezi wa kweli yaani Allah , athaari zake huwa ni nzuri na maombi huteremsha rehema za Mwenyezi Mungu.

Kila mwanadamu , mtoto au mkubwa , mwanamke au mwanamume , anastahili heshima na umuhimu katika jamii. Heshima inamfanya mtu aondokane na hisia za kujiona duni , kwani hisia za kujiona duni ni maradhi yanayomfanya mtu na hata taifa lisijitume kupata maendeleo. Ni muhimu sana kwa wazazi na walezi kupandikiza na kuendeleza hisia za heshima na kujiamini ndani ya mtoto. Kuhusiana na hilo ,wakati mmoja Mjumbe wa Allah s.a.w alisema" *Enyi watu, waheshimuni watoto wenu kwani kuwaheshimu watoto ni kinga dhidi ya jahannamu."* Sahemu nyingine Mtume s.a.w alisema " *akremu auladakum wa ahsenu adabahum"* yaani waheshimuni watoto wenu na wafunzeni adabu njema. Ni dhahiri kuwa kutokana na matamshi haya ya



Sheikh Asif Mahmood Butt

Mtume s.a.w kumkemea mtoto mara kwa mara , kumcheka cheka , na kumfanya kitovu cha mzaha , kunamfanya mtoto adhalilike . hali hii humfanya mtoto awe na chuki , akose adabu na khulka njema. Lakini mtoto akipewa heshima , ndani yake mnazaalika upendo , adabu nzuri na utii halisi. Ndiyo maana akasema waheshimuni watoto wenu na waleeni vizuri. Heshima ni haki ya kila mtu , na matokeo yake ni kupatikana kwa wema na uhusiano mzuri , na ye yote anayetendewa kwa heshima , huyo huonesha usikivu mzuri wa nasaha anazopewa na huwa na adabu njema sana. Ndiyo sababu heshima imeambatanishwa na adabu nzuri na sababu ya kutoa agizo la kuwaheshimu watoto ni kwamba matokeo yake lazima yatakuwa ni malezi mazuri.

Malezi ya watoto yanategemea pia mapenzi na mahusiano ambayo yanaleta athari nzuri sana. Mtoto huelewa jambo haraka akielezwa kwa upendo na hulikubali kwa moyo mkunjufu na kwa furaha ,ukilinganisha na kama akiambiwa kwa kukemewa . ukaali unazaa chuki , njia hii haifai kwa malezi ya watoto. Mtume wetu Mtukufu s.a.w ameonyesha mfano mwema wa kuigwa. Bi Aisha anasimulia kuwa kila mara Bi Fatima r.a.alipomtembelea Mtume s.a.w basi Mtume s.a.w alikuwa akisimama , anashika mikono yake nu kuibusu na kumkaalisha mahali pake. Vivyo hivyo Mtume s.a.w naye alipomtembelea Bi Fatima r.a. alikuwa akisimama akashika mkono wake na kuubusu na kumkaalisha katika sehemu yake ya kukaalia. Bibi Aisha anahadithia kuwa safari moja walimtembelea wageni kutoka vijijini , akawauliza , je ninyi mnawabusu watoto wenu ? wakasema : wallahi sisi hatuwabusu watoto wetu. Hapo Mtume s.a.w akasemakuwa mimi sina mamlaka yoyote kwani mmekwisha ondolea rehema moyoni mwenu. Halikadhalika Akraa bin jaabis alimwona Mtume s.a.w akimbusu Imam Husain r.a , akasema :mimi nina watoto kumilakinisijawahipokumbusu hata mmoja miongoni mwao. Mtume s.a.w akasema:yule ambaye hana huruma naye Mungu hatamhurumia.

Matendo haya ya Mtume s.a.w ni njia nzuri ya kuonyesha malezi kwa watoto ili baada ya wao kuonyesha upendo kwa wazazi wao watakuwa wepesi wa kupokea malezi mazuri.

Wasikilizaji waheshimiwa, mtoto anapofikia umri wa kujielewa na kupata fahamu nzuri , wazazi na walezi wameagizwa kuwaelekeza watoto kufanya ibada ya sala . Mtume s.a.w alisema " watoto wenu wakifikia umri wa miaka saba , wawaamrisheni wasali na tumieni ukali wanapofikia umri wa miaka kumi. Allah anasema ndani ya Qur'an Tukufu " sala huzuia mambo ya aibu na maovu." Yaani sala humsaidia mtoto kujiweka mbali na mambo ya aibu na maovu na kumwelekeza kwa njia iliyonyooka ya Mwenyezi Mungu. Kusali sala ni njia bora sana kwa ajili ya malezi ya watoto .kutokamna na ibada wanajenga sifa na tabia nzuri ndani yao na wakikua huwanufaisha sana. Wakubwa wakifuatana na watoto msikitini ni dalili ya malezi mema na mwendo huu uanzie umri wa miaka saba. Mtoto anapofikia umri wa miaka kumi , hupenda sana kujishughulisha na michezo na kughafilika kwenda msikitini. Kwa hiyo ukali utumike ikifanana na dawa chungu lakini inaponyesha na hatimaye humnufaisha kimwili na kiroho pia . Ndiyo maana hata wakati wa kula daku mwezi wa ramazani , inapendeza pia kuwaamsha watoto ili washiriki katika baraka za mwezi huu na wanapokuwa waanze kuzoeshwa ili wasipate taabu hapo baadaye. Ndugu zanguni wapendwa , Mtume s.a.w alisema kuwa hakuna zawadi bora mzazi anayoweza kumpa mwanae inayolingana na malezi mazuri. Kama vile mtoaji wa zawadi na mpokeaji wa zawadi, hufurahia kitendo hiki na haipotezwi kamwe. Vivyo hivyo malezi mema pia yana hadhi na heshima yake na yanawapa heshima kubwa sana wazazi. Mtume Muhammad s.a.w alieleza kwamba malezi mema ni zawadi na akawahamsisha wazazi wawapambe watoto wao kwa malezi bora na elimu njema . Bila shaka kazi zao hizi ni kwa dhahiri ni zaidi ya urithi wanaouacha kwa vizazi vinavyokuja badaaye. Malezi bora ni tunu yenye thamani na ni tegemeo la mustakbal wa taifa lo lote lile.

UCHAGUZI WA MAJLIS AMILA ZA MATAWI 2013 - 2016

Amir Sahib - Jamaat Ahmadiyya Tanzania, anapenda kuwakumbusha Masheikh wa Mikoa, Marais wa Mikoa, walimu wa Jamaat nchini na Wanajumuiya wote kwa ujumla kwamba sawa na kalenda ya matukio ya Jumuiya ya mwaka 2012/13 Majlis Shura ya Kitaifa itafanyika kwenye eneo la Jumuiya Kitonga - Dar es Salaam siku za Jumamosi na Jumapili tarehe 27 - 28 April 2013.

Matawi yote yantakiwa yafanye vikao vya kupendekeza ajenda za Shura pamoja na kuchagua wajumbe wa kuyawakilisha matawi yao kwenye Shura hiyo ya Kitaifa. Mapendekezo ya ajenda pamoja na majina ya wajumbe yatumwe hapa Makao Makuu kabla ya tarehe 31 Machi 2013.

Ni muhimu kila tawi la Jumuiya lisipoteze nafasi yake ya kuleta mjumbe kwani wakati wa Shura hiyo pia kutakuwa na uchaguzi wa Majlis Amila ya Taifa .

Wasifu wa Hayati Mwalimu Abdallah Ali Ng'ambage

Na Mwalimu Ali S. Ng'ambage

Mwalimu Abdallah Ali Ng'ambage alizaliwa mwaka 1932 katika kijiji cha Muhije Wilayani Liwale. Mwaka 1945 akiwa na umri wa miaka kumi na tatu wazazi wake walihamia wilaya ya Kilwa na kuweka makazi yao kijijini Mitole.

KUJIUNGA NA AHMADIYYA
Mwishoni mwa miaka ya 1958 akiwa kijana Abdallah Ali alikwenda mjini Dar es salaam na yeye bila kufanya ajizi kwa msaada wa Mwenyezi Mungu akajiunga na Jamaat Ahmadiyya mwanzoni tu mwa miaka ya 1960.

UPINZANI
Kama kawaida habari za kujiunga kwake na Ahmadiyya zilifika Kilwa Mitole baada ya kurudi nyumbani Masheikh wakajipanga kwenda kuhojiana nae lakini kwa aibu kubwa walishindwa vibaya katika hoja za dini na badala yake wakaanza kuleta maneno ya uchochezi na fitina kwa wazazi wake na ndugu wa karibu. Fitina za Masheikh hao zilionekana kufanikiwa sana kwa baadhi ya ndugu kwani baadhi yao walianza kumkwepa katika kusalimiana nae pamoja na kumzuilia uongo wa aina mbalimbali. Lakini hali hiyo ilikuwa tofauti kwa wazazi wake yaani kwa baba yake Mzee Ali Ng'ambage na mkewe. Wao hawakuona kosa la mtoto wao hivyo waliendelea kuwa nae bila kinyongo chochote na kufanya fitina za maadui kwa wazazi wake zigonge ukuta.

Hali ilikuwa ya faraja sana kwake pale ambapo kaka yake Bw. Salum Ali Ng'ambage alipojiunga na Ahmadiyya. Hata baba yao alipofariki maadui walitaka kuwazuia kumzika lakini kwa msimamo imara wa mama zao na dada zao japo hawakuwa Waahmadiyya walihakikisha kaka zao hao hawatengwi katika mazishi ya baba yao.

KAZI YA MAHUBIRI
Mwanzoni mwa miaka ya 1960 kijana Abdallah Ali Ng'ambage alianza kazi ya kuhubiri dini baada ya kupata elimu ya dini pale Masjid Salaam Mnazi Mmoja Dar es salaam. Ninakumbuka sana baadhi ya maeneo aliyowahi kuhubiri hapa nchini. Hadi 1966 alihubiri Tanga 1967 - 1968, Mwanza 1969 - 1970, Tabora 1971 - 1973, Newala 1974, Mtwara 1975 - 1980, Kilwa Kivinje 1981 hadi 2006. Pia alihubiri katika m aeneo ya Kibiti, Machame na Kilwa Masoko.

Katika kazi yake ya mahubiri Mwalimu alikumbana na matatizo mengi sana licha ya upinzani wa manenoo ya matusi na kashfa dhidi yake kutoka kwa maadui wa Ahmadiyya kama ilivyokawaida kwa Waahmadiyya wote pia katika maeneo mengine alipigwa, mathalani Tanga alipigwa chuma kichwani, Tabora na maeneo ya Newala alipigwa mawe na pale Kilwa yupo jamaa alidiriki kumshikia kisu na kutaka kumchinja. Nakumbuka kuna wakati alisokolewa, alizomewa na hata kutemewa mate hata mimi (mwandishi) nilizomewa na wanafunzi wenzangu shuleni baada ya Mwalimu mmoja wa kisuni kuwaamuruwanafunzi wanizomee kwa sababu baba yangu ni Kadiani (kafiri) hayo yalitokea mwaka 1976 shule ya msingi Kinyonga - mjini Kilwa Kivinje.

Pamoja na yote hayo Mwalimu Abdallah Ng'ambage hakuonyesha kukasirika au kukerwa na yote hayo badala yake kila kukicha yeye kiguu na njia vitabu na magazeti mkononi kwa maneno ya upole na laini akihubiri na kutangaza ujumbe wa Seyyidna Ahmad a.s. bila woga wala hofu. Mahubiri yalikuwa ndani ya damu yake. Alifikisha ujumbe wa Seyyidna Ahmad a.s. kila kona na kwa msaada wa MwenyeziMungu watu wengi wamejiunga na Ahmadiyya kupitia mahubiri yake. Mwalimu Abdallah Ng'ambage hakuwa mtu wa kupoteza muda kwa ajili ya maongezi ya mambo ya kidunia kama mipira au siasa n.k bali yeye muda mwingi maongezi yake ni juu ya dini na hasa shughuli mbalimbali zinazofanywa na Jumuiyya ya Ahmadiyya. Alipenda sana kusimulia habari za watu walioipenda na kuitumikia dini kama akina Sheikh Kaluta Amri Abedi, Maulana Sheikh Muhammad Munawwar na wahubiri wenzake akina Mwalimu Daudi Shhoo, Mwalimu Abdu Imran n.k

Hata baada ya kustaafu kazi aliendelea kuwa katika hali hiyo alidumu katika ibada mpaka siku ya mwisho wa maisha yake. Nakumbuka katika siku zake za ugonjwa aliniambia tena kwa kusisitiza kwamba yatupasa tuelewe kwamba yeye ni Ahmadiyya hivyo tusithubutu kumpa dawa ambazo haziendani na mafundisho ya dini. Hayo aliyasema baada ya kuletewa dawa fulani za miti shamba. Nilimtoa hofu kuwa hatutaweza kufanya hayo kwani sote sisi tunafahamu hayo.

KIFAMILIA
Ukiondoa shughuli za mahubiri, kifamilia alikuwa ni mtu mwenye huruma sana kwa ndugu, watoto na majirani zake. Alionyesha njia ya kusaidia hata pale ambapo yeye mwenyewe hana kitu, alikuwa mkweli na hakuwa mtu wa kupenda makuu.

KIFO CHAKE.
Siku moja kabla ya kifo chake



Abdallah Ali Ng'ambage enzi za ujana wake

tukiwa mimi, mkewe binti Issa na mwanae Maimuna alituambia kuwa yeye alijiunga na mpango wa Wasia na kwamba akifa maiti yake izikwe katika maeneo ya makaburi ya Jamaat kule Temeke. Aliyasema hayo dakika chache tu kabla ya homa iliyomsababishia kifo chake kuanza. Lakini kutokana na taarifa kutofautiana haikuwezekana kuzikwa Temeke badala yake akazikwa kwa mwanae Ikwiriri Rufiji.

Mwalimu Abdallah Ng'ambage alifariki siku ya Jumatatu tarehe 24/09/2012 na kuzikwa tarehe 25/09/2012 Jumanne. Mwalimu ameacha wake wanne na watoto 19.

Dua natakabalia Mola Mrehemu baba Mwl. Abdallah Ali Ng'ambage (Amin).

MOLA MREHEMU
BABA ABDALLAH ALI
NG'AMBAGE

1 Twakuaga wetu bwana,
Mwalimu Abdallah Ali
Umekwenda kwa Rabana,
akhera nyumba jamili
Huzuni imetubana,
kwa kwikwi twalia kweli
Mola mrehemu baba,
Abdallah Ali Ng'ambage

2 Kwa heri wetu mpenzi,
baba yetu wa thamani
Metuachia majonzi,
wanao na wanandani
Safariyo nyemelezi,
tutakuona ndotoni
Mola mrehemu baba,
Abdallah Ali Ng'ambage

3 Baba tunakukumbuka,
kwa yako mengi mazuri
Ulimwogopa Rabbuka,
haukuwa mjeuri
Maisha yako hakika,
yalikuwa yenye kheri
Mola mrehemu baba,
Abdallah Ali Ng'ambage

4 Baba ulikuwa mwema,
kwa ndugu na majirani
Kwa nyingi zako heshima,
wengi walikuamini
Leo tumeshika tama,
hatukuoni machoni
Mola mrehemu baba,
Abdallah Ali Ng'ambage

5 Ulikuwa usukani,
familia kuongoza
Ulituweka nuruni,
mema kutuelekeza
Wenye majonzi moyoni,
wewe ulibembeleza
Mola mrehemu baba,
Abdallah Ali Ng'ambage

6 Ulikuwa mbele sana,
dini kuikamatia
Ulifanya mengi sana,
kila pembe watambua
Ulipambana kwa kina,
dini kuipigania
Mola mrehemu baba,
Abdallah Ali Ng'ambage

7 Dini ulitumikia,
hukuitaka dunia
Miguu ulitumia,
watu kuwafikishia
Mungu Alikujalia,
ulimi kuutumia
Mola mrehemu baba,
Abdallah Ali Ng'ambage

8 Majeraha ulipata,
kupigwa chuma kichwani
Mawe yalikuparata,
damu kuvuja mwilini
Hata hivyo hukusita,
kuipigania dini
Mola mrehemu baba,
Abdallah Ali Ng'ambage

9 Tanga Mwanza na Tabora,
sautiyo ilifika
Machame Lindi Mtwara,
wote wanakukumbuka
Ulihubiri kwa ghera,
kwa msada wa Rabbuka
Mola mrehemu baba,
Abdallah Ali Ng'ambage

10 Wa Mmeda, Luagala,
Salamu zipokeeni
Chitandi kule Newala,
Nanyi twawajulisheni
Litehu na Luagala,
Ng'ambage hatumuoni
Mola mrehemu baba,
Abdallah Ali Ng'ambage

11 Ulifanya mengi mema,
pepo kujiandalia
Kutwakutwa hata kama,
hayeshi kusimulia
Yanibidi kusimama,
sifazo kuhadithia
Mola mrehemu baba,
Abdallah Ali Ng'ambage

12 Tutakuenzi kwa mema,
ya utumishi wa dini
Tunamuomba Karima,
na sisi tuwe kundini
Kwenye dini kuchegama,
daima tuwe vitani
Mola mrehemu baba,
Abdallah Ali Ng'ambage

13 Baba yetu umefika,
akhera kwenye thamani
Wala hatuna mashaka,
hutoingia motoni
Mola wetu msifika,
Atakupa afueni
Mola mrehemu baba,
Abdallah Ali Ng'ambage

14 Kwa hapa naishilia,
kalamu naweka chini
Sitoweza endelea,
machozi tele machoni
Baraka namuombea,
amghofiri Manani
Dua natakabalia,
Mola mrehemu baba

Ali S. Ng'ambage (Teacher)
Njinjo - Kilwa.

UCHAGUZI WA MAJLIS AMILA ZA MATAWI 2013 - 2016

Amir Sahib - Jamaat Ahmadiyya Tanzania, anapenda kuwajulisha Masheikh wa Mikoa, Marais wa Mikoa, walimu wa Jamaat nchini na Wanajumuiya wote kwa ujumla kwamba sawa na maagizo kutoka Markaz, mwaka huu 2013 ni mwaka wa uchaguzi wa Majlis Amila zote za matawi nchini kote.

Hivyo Masheikh, Walimu na Marais wa mikoa, wanaagizwa kusimamia chaguzi za Majlis Amila za matawi yote yaliyomo katika maeneo yao. Chaguzi hizo zifanyike kati ya mwezi Februari na mwanzoni mwa Aprili 2013 na ripoti zitumwe Makao Makuu Dar es Salaam kabla ya Shura ya Kitaifa.

Mnasisitizwa kuzingatia kanuni zote za uchaguzi sawa na mwongozo wa Jamaat.

Bustani ya Washairi

DUNIA NA'ALABUKU - KAMWE HAINA SALAMA

1. Naanza Bismillahi, Arahmani Rahimu
Ni Jina Lako Ilahi, Mwenyezi Mungu Karimu
Utunzi uwe swalihi, unoge uwe mtamu
Dunia Na'alabuku, kamwe haina salama.

2. Maakuli ya mseto, ya wakubwa na makamu
Kinofaa kwa watoto, akina mama na amu
Kisikupite si moto, ni barakatu naimu
Dunia Na'alabuku, kamwe haina salama.

3. Dhamiri yangu na nia, ile nilokusudia
Kuelezea Dunia, tunavyo papatikia
Khatima twadidimia, mkondoni maasia!
Dunia Na'alabuku, kamwe haina salama.

4. Dunia yakhe dunia, ina mengi mengi sana
Yapo Mola Aridhia, tuyafanye kwa mapana
Mengine katuambia, tuache mana hayana
Dunia Na'alabuku, kamwe haina salama.

5. Dunia ina kinaya, kinai usiifate
Imesheheni mabaya, imejaa kotekote
Si mambo bali kayaya, na tuyatemee mate
Dunia Na'alabuku, kamwe haina salama.

6. Bali hawaa hujiri, hushawishi ya laana
Yale mambo ya khatari, ya kumuasi Rabana
Na mtu huwa twayari, kwa usiku na mchana!
Dunia Na'alabuku, kamwe haina salama.

7. Khasa pale pa ujana, Dunia bibi Arusi
Kila kizuri waona, kiwe chako cha nemsi
Vibaya vilivyonona, havioneki kinyesi
Dunia Na'alabuku, kamwe haina salama.

8. Dunia inayo adha, kubwa isiyo kifani
Hufika kadha wa kadha, humu mwetu maishani
Ibada huwa ni fedha, bali hatuithamini!
Dunia Na'alabuku, kamwe haina salama.

9. Dunia husaulisha, kwa mshika madaraka
Raia akayumbisha, patashika na mashaka
Bali mwisho wa maisha, naye huja kuteseka!
Dunia Na'alabuku, kamwe haina salama.

10. Akatendwa alotenda, au zaidi ya vile
Ndipo humpondaponda, pakawa pa maji male
Uwezo wa kujilinda, akawa hanao yule
Dunia Na'alabuku, kamwe haina salama.

11. Mbali usijitanibu, tazama usighuriwe
Uwe karibu karibu, Subhana Umjuwe
Jivishe hiyo hijabu, akhera uokolewe
Dunia Na'alabuku, kamwe haina salama.

12. Unategemea nini, ewe mtu kama mimi?
Ibada huithamini, na nini utajihami?
Haifai talakini, hufui dafu utemi
Dunia Na'alabuku, kamwe haina salama.

13. Dunia siyo swahibu, mwema wa kuenda nayo
Kila wakati jaribu, kukwepa iliyo nayo
Khasa khasa ya dhunubu, yale yaangamizayo
Dunia Na'alabuku, kamwe haina salama.

14. Dunia uitazame, kwa mapana na marefu
Yamo ndanimwe mahame, yanayotoa harufu
Hayahitaji usome, yapo wazi ni machafu
Dunia Na'alabuku, kamwe haina salama.

15. Twende kwa uangalifu, tukiangalia chini
Tukimuomba Raufu, Atuchopowe motoni
Tuusome Msahafu, tutwalii Quruani
Dunia Na'alabuku, kamwe haina salama.

16. Jengo letu la Akhera, tulijenge kwa tofali
Kwa nafsi ya twahara, swala na njema amali
Tusipoteze majira, tukumbuke jambo hili
Dunia Na'alabuku, kamwe haina salama.

Al-Ustadhi Khamisi S.S. Wamwera
Kimbangulile - Mbagala Rangi Tatu
S.L.P 376 dar es salaam.

LA KHERI LISIPOTIMU

1. Ukiifanya juhudi, ya kheri kuifikia
Tena kwa umaridadi, na sala kuongezea
Kisha ifike kipindi, mambo yakakuchachia
Huenda hapo wadudi, baya kakuepushia
La kheri lisipotimu, lina shari ndani yake

2. Kila ukijitahidi, haraka kuyafanyia
Muda unataradadi, mambo yazidi kawia
Mwenyezi Mungu Majidi, Yeye ndiye anajua
Pengine yangekuzidi, mwishoni yakakuua
La kheri lisipotimu, lina shari ndani yake

3. Usije hama baladi, pindi inapotokea
Kwa kuwa uliahidi, na watu walingojea
Mola sio Mkaidi, zuri kakuandalia
Kakwepusha vya gaidi, visije kukulipua
La kheri lisipotimu, lina shari ndani yake

4. Usimsake hasidi, aliyekuvurugia
Utaongeza idadi, ya unaowachukia
Cha msingi ni kurudi, Kwa Mola wako Jalia
Ili uje kufaidi, katika vya awalia
La kheri lisipotimu, lina shari ndani yake

5. Adhana yake madadi, kwa mbali naisikia
Acha nenda Masjidi, dhuhuri imeingia
Kisha Bi Radhia Abedi, haliye kumjulia
Kwa Ng'amilo sina budi, jioni nitapitia
La kheri lisipotimu, lina shari ndani yake

Twahir Mahmood Hamsini Mubiru
(Mkono shavuni)
S.L.P 376 Dar es salaam

KIFO CHA NABII ISSA (AS)

1. Salamu Aleikumu, ndugu zangu waumini
Hizi ni zangu salamu, naomba zipokeeni
Na baada ya salamu, kheri nawatakieni

Kifo cha Nabii Issa si jambo la kushangaza

2. Issa mwana Mariyamu, ni kweli amefariki
Na kwa kila mwanadamu, kifo hakikimbiliki
Issa aleisalamu, kaenda mbele ya haki
Kifo cha Nabii Issa si jambo la kushangaza

3. Yesu apae mbinguni, ni jambo la kushtuka
Hivi ni Nabii gani, aliyevuka mipaka
Mipaka ya Quruani, Mola Aliyo iweka
Kifo cha Nabii Issa si jambo la kushangaza

4. Huyu ni Nabii wetu, na kweli anasifika
Lakini tusithubutu, kuja kuvunja mipaka
Dhana itoke kwa watu, kifo yeye kuepuka
Kifo cha Nabii Issa si jambo la kushangaza

5. Kama kupaa mbinguni, angepaa MuhammAdi
Ni Nabii mwenye shani, wengineo kawazidi
Lakini Mola Manani, alisha weka ahadi
Kifo cha Nabii Issa si jambo la kushangaza

6. Someni sura ya tano, Aya sabini na sita
Hilo litakuwa somo, na ukweli mtapata
Si bali tu minong'ono, huku aya mwazitupa
Kifo cha Nabii Issa si jambo la kushangaza

7. Quruani kuisoma, yataka wenye mwongozo
Tena wale wenye homa, ya kutaka mwendelezo
Na kama huna hekima, utaanzisha vikwazo
Kifo cha Nabii Issa si jambo la kushangaza

8. Aya thelathina nne, sura ya kumi na tisa
Hii ni hoja nyingine, kifo kilimtikisa
Mkazisome muone, msije sema nazusha
Kifo cha Nabii Issa si jambo la kushangaza

9. Ushahidi upo mwingi, tena upo mwingi sana
Quruani ndo msingi, mkisoma mtaona
Hizi ni fadhila nyingi, katujalia Rabana
Kifo cha Nabii Issa si jambo la kushangaza

10. Beti kumi naishia, ujumbe upokeeni
Yafaa kuzingatia, na msome Quruani
Ili mpate kujua, kinachoelezwa nini
Kifo cha Nabii Issa si jambo la kushangaza

Hamidu Liucha
S.L.P 788 Morogoro (Jamia)

AMANI HAIPATIKANI BILA YA AHMADIYYA

1. Ahmadiyya ni nini, ndugu zangu nauliza?
Watu waliomakini, hawatumii miujiza
Walianza Qadiani, kijijini kwa Miriza
Umetufahamu nani, kabla sijamaliza
Kama wataka amani, jiunge Ahmadiyya

2. Amani ni utulivu, kimwili hata kiroho
Haihitaji mabavu, kuifurahisha roho
Usitumie miguvu, na usiwe na kihoro
Utabakia mafuvu, kijifanya horohoro
Kama wataka amani, jiunge Ahmadiyya

3. Tunapenda utulivu, tukiwa mahala popote
Wapole sana kama jivu, hatushindwi na chochote
Muulize hata Munibu, mpole wakati wote
Tumefunzwa na mababu, tunaheshima kwa wote
Kama wataka amani, jiunge Ahmadiyya

4. Tunafanya mahubiri, kwa upole mahsusi
Ni matamu si shubiri, muulize bwana usi
Tunakuwaga mahiri, hatutumii matusi
Walimu wetu wazuri, wamejawa ikhlasi
Kama wataka amani, jiunge Ahmadiyya

5. Nidhamu yetu imara, tangu mwaka themanini
Walikuwepo vinara, watu walio makini
Hatuwagi na papara, kwenye mambo ya imani
Kama wataka amani, jiunge Ahmadiyya

6. Shekhe wetu Mubaraka, kaileta Jumuiyya
Alikuja kwa baraka, za Mwenyezi nakwambia
Akajifunga mkaka, na malengo kufikia
Nidhamu akamulika, Tabora akaingia
Kama wataka amani, jiunge Ahmadiyya

7. Waislamu wezetu, Hawanaga mikutano
Sisi huwa jadi yetu, tunakusanyika mno
Watulivu roho kwatu, tutii bila mfano
Ukitaka njoo kwetu, utapata sala tano

Kama wataka amani, jiunge Ahmadiyya

8. Tukiuona ugomvi, tunapatwa na huzuni
Hatuongezei chumvi, tunatema mate chini
Kama watu wenye mvi, watauliza kunani
Msiwe kama shomvi, karibuni kundini
Kama wataka amani, jiunge Ahmadiyya

9. Tunaishi kwa upole, kwenye nyumba za kupanga
Muulize Ndendekile, aliyeanza kupanga
Kwenye chumba kilekile, maeneo Keko Mwanga
Mkewe pia mpole, hana maneno ya kanga
Kama wataka amani, jiunge Ahmadiyya

10. Sikiliza kwa makini ewe usiyeko ndani
Haya yote ni madini, meyatoa kibindoni
Ukhalifa umo ndani, ulianza Qadiani
Umedhihiri kwa shani, bado upo duniani
Kama wataka amani, jiunge Ahmadiyya

11. Wenye Khalifa ni sisi, twamshukuru Manani
Ahmadi Muasisi, kazaliwa Qadiani
Hiyari yake Qudusi, kumuotesha ndotoni
Mara zote hatuasi, pamoja maisha duni
Kama wataka amani, jiunge Ahmadiyya

12. Hatuamini majini, kama unayo yaleta
Huo ni ufirauni, wengi wauvaa pete
Ukiuliza ya nini, anajiliza na bwete
Namuogopa Manani, simuogopi yeyote
Kama wataka amani, jiunge Ahmadiyya

13. Niwapeni siri moja, ndugu ninaowapenda
Sisi tunao umoja, ndo maana tunapanda
Jitahidi moja moja, we mwenyewe utapenda
Njoo ujifunze hoja, za wateule wapendwa
Kama wataka amani, jiunge Ahmadiyya

14. Nimefikia mwishoni, bado niko kilingeni
Wengi hamuwaoni, wana mengi ya kundini
Ba!! ngoja niwapisheni, nikapumzike chini
Kimbilieni kundini, huko mnangoja nini?
Kama wataka amani, jiunge Ahmadiyya

Abdallah Kalindima (K-mtoto)
S.L.P 376 Dar es salaam

"Mwelewe Maulvi Nuruddin"

Hadhrat Khalifatul Masih I r.a.

Hiki ni kitabu kilichoandikwa na Sir Muhammad Zafrullah Khan r.a. na kutafsiriwa kwa Kiswahili na Sheikh Jamil Rahman Rafiq

Kutoka toleo lililopita

KUMBUKUMBU YANGU

Hilo likanivutia, lakini upendo wa babangu ulikuwa bora zaidi.

Baada ya alasiri, Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. alikuwa anapenda kukaa katika behewa la nyumba yake ndogo ambalo wakati huo katika saa za mchana lilikuwa na baridi kidogo ya kufaa. Huko pia nikakaa naye. Siku moja akasema: "Hizi ni saa za kucheza.» Hutaki kushiriki katika mchezo wowote?"

Nikasema kwa heshima: "Mpenzi, nina furaha sana hapa nilipo."

Halafu nikatakiwa kumwomba ruhusa niende kwetu nikajitayarishe kwa safari yangu ya kwenda Uingereza. Mama yangu akahofia mtengano mrefu ujao, nami nikajikunyata kwa kujitupa pasipojulikana na kwenda kushinda kule nilikojua kidogo, na hicho kidogo pia cha uvumi tu, kukaa na watu ambao imani yao, utamaduni wao na namna walivyoishi ni tofauti kabisa na ile yangu. Kwa hiyo kujitayarisha hakukuwa na msisimko, na nikashikwa na fadhaa nyingi na wahaka.

Safari yangu iliandikishwa toka Bombay hadi Trieste na meli ya Austrian Lloyd iliyopangwa kung'oa nanga Septemba 1, 1911. Wazazi wangu, babangu mdogo na hadimu wa familia wakaondoka Sialkot asubuhi na mapema tarehe 28 Agosti kwa garimoshi kwenda mpaka Batala na wakawasili Qadian jioni. Nikamwomba ruhusa Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. keshoye. Akaagana nami kwa upendo na maombi. Akaniandikishia maagizo kadha na maombi ambayo nikaandika; pia akanipa nasaha kwa mdomo. Akaniagiza nimwandikie mara kwa mara. Mama yangu akafurahi sana kuonana na Hadhrat Ummul Muminin. Tukaondoka Qadian jioni hiyo kuelekea Batala na kupanda garimoshi kwenda Amritsar ambako mamangu, baba mdogo na hadimu walifunga safari ya garimoshi kuelekea Sialkot; babangu na mimi tukachukua treni ya posta (garimoshi linalochukua barua pia, na linakwenda kwa kasi) kwenda Bombay, umbali wa maili elfu moja. Nilikuwa sijasafiri kupitia Amritsar hapo kabla, kwa hiyo kutoka hapo kila kitu kilikuwa kipya kwangu. Tukawasili Bombay Agosti 31, na keshoye saa sita za mchana nikaingia meli ya S.S. Koerber, yenye kuhamisha maji tani 4,000. Babangu akapeana mikono nami kama alama ya kuagana, chini ya ubao wa kuingilia melini; na zaidi ya kupeana mikono hata neno moja halikusemwa na sote wawili.

Haikupita saa baada ya meli kuondoka nikapatwa na ugonjwa wa taabu ya bahari (kuchafuka tumbo na kutapika chomboni), hali ambayo sikuhadharishwa nayo kabla wala sikuijua. Upepo wa kusi ulikuwa ukivuma kwa nguvu zote na siku nne zijazo zilikuwa za taabu kubwa kabisa isiyofifia ya kufadhaisha. Tulipotoka tu eneo la upepo wa kusi, kila kitambo cha safari kikathibitika cha kufurahisha. Baada ya kutokula kwa siku nne nikasikia njaa kali sana, nikafurahia kila mmego wa chakula kizuri sana kilichotolewa melini. Tukawasili Trieste jioni ya Septemba 14, tukasafiri upande wa kaskazini kwa garimoshi liendalo mbio sana kuelekea Ostende, tukavuka hadi Dover na kuwasili London asubuhi ya Septemba 16.

London ilikuwa mji mkuu wa dunia nzima siku hizo. Kwa kuacha waliofilisika wenye hali ya chini sana, maisha yalikuwa mazuri na ya kuburudisha na yaliendelea bila shida. Nilikuwa na bahati sana kupatiwa makazi kama mgeni wa kulipa na watu fulani waliothibitika kuwa wapole sana walionitendea kwa ukarimu na huba sikuzote. Niliazimu kusoma sheria, na muda si muda nikajiona niko kwetu isipokuwa nilikuwa mbali na wazazi. Nikawaandikia kila wiki na kujibiwa nao kila wiki. Pia nikamwandikia Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. kama kawaida naye akanipa heshima kwa kunirudishia majibu kwa upendo akiandika kwa mkono wake. Nikamwandikia chochote nilichokuta cha kuvutia bila kusita, naye akinijibu akadhihirisha moyo wa kupenda sana kile nilichomwandikia. Haikupita kitambo kirefu nikawa napenda kusafiri; nikapitisha likizo nje ya London, lakini kila nilipotaka kwenda nje nikapata ruhusa kwake. Katika barua zake akanisalimia kwa upendo. Wakati mwingine aliniandikia kwa kuniombea:

"Mungu Akufanye uwe Zafarullah Kweli (yaani ufaulu kwa fadhili ya Mungu), au uongozwe na Mungu na uwe mwenye bahati njema."

Barua yake ya Septemba 16, 1913 niliyoandikiwa imekwisha chapishwa. Naandika hapa tafsiri yake kama mfano:

"Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

Twamhimidia Yeye, na kumsalia Mjumbe Wake Mtukufu.

Assalamu alaikum wa rahmatullahi wa barakatuh.

Mfikishie maamkizi



Maulana Hadhrat Hakeem Nuruddin Khalifatul Masih I r.a.

yangu ya upendo sana Muhammad Akbar Sahib: *Assalamu alaikum.* Haya ni maamkizi yenye baraka. Ni masikitiko kwamba Waislamu wa India hawayajali.

Kila safari yapaswa kuwa na shabaha, iwe ya kidunia au ya kidini. La sivyo, ni bure.

Mungu Aujalie msikiti katika Petersburg kuwa chanzo cha baraka.

Huko Finland nyakati za sala na saa za saumu zitapangwa kwa masaa. Mungu Amesema: Na mwezi Tumeupimia vituo (36:40). Hiyo ni kwa kuwaongoza waishio katika nchi za aina hiyo.

Fikiria sana, E Mpenzi, ya kwamba bajeti ya Kanisa la Uingereza yafikia pauni milioni ishirini na nne za Kiingereza. Kama wao hawauamini Ukristo, mbona wanatumia fedha nyingi sana hivyo kama maji?

Kwa nini nchi za Balkan, Italia na Ufaransa zilimwaga sana damu katika Uturuki, Tripoli na Moroko, kwa kupinga Islam, katika miaka miwili iliyopita?

Hoja haiisaidii itikadi ya Utatu, ambayo yaweza kumtuliza mtu mwenye akili. Kurudi nyuma kwa dini hiyo kunafungamana na Masihi Aliyeahidiwa a.s. Wafuasi wake ni watupu kwa undani wao, lakini wanasita kukubali Islam hadharani.

Unapaswa kukazania kueneza Umoja wa Mungu. Itatosha kuwafikishia wanafunzi wa Kipanjabi na wa Kihindi jina la Allah na la Mjumbe Wake.

Usilegee kusali, soma Qur'an Tukufu kwa kawaida, na daima ufanye maombi.

Amekuwaje rafiki yako Mjerumani? Hukuandika yu hali gani. Nashangaa.

Wasalamu

Nurudin"

Khwaja Kamaluddin alikuwa mwanajumuiya maarufu wa Kiahmadiyya. Alikuwa mwanasheria. Alifanya kazi ya kuwa wakili kwa muda fulani mjini Peshawar na akahamia Lahore. Yeye mara nyingi alisema kwamba wakati fulani alipata kuvutika sana na Ukristo, lakini bahati yake njema ikamkutanisha na Masihi Aliyeahidiwa a.s., ambaye chini ya uongozi wake akaimarika imani yake katika Islam naye akawa Mwislamu mwaminifu. Masihi Aliyeahidiwa a.s. alipokuwa Lahore katika matembezi yake ya mwisho na alikuwa akikaa katika Ahmadiyya Buildings, Khwaja Kamaluddin akaona katika ndoto kwamba amekamatwa na polisi pamoja na Maulawii Muhammad Ali na Waahmadiyya wengine watatu au wanne. Wakaambiwa kwamba wana hatia ya uhalifu na watapelekwa mbele ya mfalme. Wakaongozwa kwenye ukumbi mmoja mkubwa ambamo katika sehemu yake ya mwisho Maulawii Nuruddin r.a. akakaa juu ya kiti cha kifalme kilichowekwa juu ya jukwaa chini ya kipaa. Yeye akawaambia: "Nyinyi mmefanya maasi dhidi yangu. Niwatendeje?" Khwaja Kamaluddin akajibu: "U mfalme sasa, waweza kututenda upendavyo." Hapo Maulawii Nuruddin r.a. akasema: "Mnahukumiwa kufukuzwa nchini"

Khwaja Kamaluddin akamweleza Masihi Aliyeahidiwa a.s. ndoto yake, ambaye akamsitisha akisema kwamba ndoto hiyo haitabiri msiba kwake. Halafu bwana huyo akamweleza Maulawii Nuruddin r.a. ndoto yake, ambaye akazama katika fikira kwa kitambo kidogo, kisha akamwonya asimweleze yeyote ndoto yake. Baada ya siku chache Masihi Aliyeahidiwa a.s. akafariki na Khwaja Kamaluddin akamwendea Maulawii Nuruddin r.a. na kasema: Wakati wa ndoto yangu kutimia umewadia. Niko tayari kufanya baiati kwako. Akaambiwa asubiri mpaka wajumbe wa Jumuiya wapate nafasi ya kukusanyika Qadian na kuweza kushauriana.

Halafu baada ya Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. kutangazwa kuwa *Khalifa* na kuchukua majukumu ya kazi yake tukufu, Khwaja Kamaluddin akaota tena ndoto hiyo, kwa tafauti hii kwamba safari hii Hadhrat Khalifatul Masihi, alivyokuwa sasa, akamhukumu akisema: "Umeasi mara ya pili. Naamuru ukatwe kichwa." Katika ndoto Bwana Khwaja akapelekwa pale penye kuuawa. Na shoka lililopigwa na mwenye kumkata kichwa lilipoanguka juu ya shingo yake akazinduka kwa hofu.

Mnamo mwaka 1912 mkewe Khwaja Kamaluddin alifariki; yeye akapatwa na huzuni ya kupita kiasi. Fikara zake zikaelekea zaidi kwenye dini na akafunga safari ndefu kwa shabaha ya kuhutubia juu ya Islam. Alipowasili Bombay, tajiri mmoja mwungwana wa Hyderabad Dakkan, aliyeelekezwa vyema kwenye Uahmadiyya, akamwomba kutekeleza kazi yake fulani ya siri iliyohusikana na mambo ya nyumbani na aende Uingereza kwa kuitimiza. Akaahidiwa ada kubwa. Kazi yenyewe ilihusikana kidogo na sheria, wala haikuwa na matata, basi hakuwa na haja abembelezwe kuikubali. Akawasili Uingereza karibu ya mwisho wa mwaka 1912. Baada ya kutimiza kazi yake hiyo akanuia kukaa Uingereza na kujitolea kwa kazi ya kuzagaza na kuhudumia Islam. Huko Uingereza wakati huo kulikuwa na Waahmadiyya watatu tu. Mmoja alikuwa anajifunza udaktari kule Newcastle, Dkt. Ibadullah alikuwa anashughulikia kozi ya masomo ya juu katika udaktari wa meno, na mimi nilikuwa nasoma sheria. Baada ya Khwaja Sahib kuwasili, Dkt, Ibadullah akajikalifu kumpatia makazi kwa kusumbuka na kutaabika sana katika nyumba alimoishi. Upande wake, Khwaja Sahib akaazimu kuishi kikawaida, hakujali kupata chakula kizuri, nguo nzuri na kadhalika. Lakini haukupita muda mrefu, chumba chenye kufaa kikapatikana katika nyumba nilimoishi, naye akahamia humo. Hivyo, tukashirikiana sana kwa muda wote aliokaa nasi, nami nikapata kumjua vizuri sana. Siku hizo akafikiria kuanzisha jarida la kila mwezi alililoliita *"Muslim India and Islamic Review"*. Baadaye "Muslim India" ikaachwa katika jina lake na likaendelea kutolewa kwa miaka mingi kwa jina *"Islamic Review."* Maongezi yetu kwa kawaida yakawa kuhusu Islam na Uahmadiyya ambamo Khwaja Sahib akatangulia. Hivyo nikapata ujuzi wa mambo fulani ambao nisingeupata bila kuongea naye.

Safari moja, kwa mfano, akasema: "Maulawii akifa, (mara nyingi akasema Maulawii kwa ukunjufu na huba akimaanisha Hadhrat Khalifatul Masihi r.a.) hakuna budi matatizo kutokea kuhusu kumteua atakayekuwa *Khalifa* mahali pake. Hebu tuone sasa. Yupo Mahmud, (akimaanisha Sahibzada Mirza Bashiruddin Mahmud Ahmad r.a.) lakini yu kijana tu mdogo; na yupo Muhammad Ali, yeye si mvumilivu hata kidogo, huanza kupiga kelele juu ya kila jambo dogo. Ama mimi, nashindwa kujizuia kufoka kweli, ikifaa, isipofaa."

Kwa bahati mbaya, nilivyojua habari zake, wakati mwingine nikapenda anihakikishie kweli anaudhika sana. Lakini nikafikiri kwamba pengine anachukua maana fulani ya ukweli iliyo tofauti

Endelea uk. 8

"Mwelewe Maulvi Nuruddin"

Hadhrat Khalifatul Masih I r.a.

Kutoka uk. 7

na ile yangu. Kuhusu swala la *Khalifa* baada ya kufariki Khalifatul Masihi wa kwanza, nikamkumbusha kwamba ni jambo ambalo haujafikia wakati wake, tena halina haja ya kujadiliwa. Hadhrat Khalifatul Masihi amekariri kuhakikisha kwamba wakati ukiwadia Mungu Mwenyewe Ataamua na kumfanya *Khalifa*.

Safari moja Khwaja Sahib alisumbuka sana mno kwa kushuhudia mandhari fulani iliyomkumbusha ndoto yake ambamo akaota yuko tayari kukatwa kichwa. Alikuwa na uchungu mkubwa wa kutisha hata kwamba bila kujua sababu yake nikahuzunika. Baada ya kitambo alipopata kutulia, akanieleza ndoto zake.

Dkt. Henry Leitner, mtaalamu wa elumu ya nchi za mashariki, alikuwa Mwalimu Mkuu wa Oriental College, Lahore, mnamo miaka ya mwisho ya karne ya kumi na tisa. Kwa kutumaini kustaafu akapanga mpango wa kuanzisha Idara ya Elimu ya Nchi za Mashariki katika au karibu ya London, na akawaendea watawala Waislamu wa maeneo mbalimbali ya India ili waichangie hiyo idara. Miongoni mwa waliotoa michango mikubwa walikuwepo Mtukufu Begum wa Bhopal, mtu mwenye cheo cha kwanza na Waziri Mkuu wa Hyderabad, Nawab Sir Salar Jang. Akirejea Uingereza, Dkt. Leitner akachagua na kununua eneo kubwa la ardhi karibu ya Woking, katika Surrey, kwa mpango wake na akaanzisha ile Idara ya Elimu ya Nchi za Mashariki katika eneo hilo, na pia akajenga msikiti mdogo na nyumba katika sehemu ya eneo hilo. Msikiti ukaitwa Shah Jahan Mosque kwa jina la Begum wa Bhopal, na nyumba ikaitwa Sir Slaar Jang Memorial House. Woking iko umbali wa maili ishirini na nne kutoka London. Kwa kuwa huko Woking wala karibu yake hawakuwepo Waislamu, sala hazikusaliwa katika msikiti huo na ukawa kama nyumba ya makumbusho, au kitu cha sanaa ya ujenzi kwa wanye kuzuru.

Dkt. Leitner alipofariki, mali hiyo yote ikamilikiwa na watu wa familia yake na ikaja chini ya usimamizi wao. Karibu wakati huo, Seyyid Amir Ali, Jaji wa Korti Kuu ya Calcutta, Mwislamu mwenye moyo wa kufadhili watu kuliko nafasi yake na mtaalamu mashuhuri, aliyejulikana kwa vitabu vizuri alivyotunga, *The Spirit of Islam and History of Saracens,* akafanywa kuwa mwanakamati wa kamati ya wanasheria ya Baraza la Mtukufu Mfalme, na akaanza kukaa London. Mwislamu mwingine mashuhuri katika London wakati huo alikuwa Mirza Abbas Ali Beig aliyekuwa mshauri mmojawapo wa Baraza la washauri la Katibu wa Utawala kwa India. Hao wawili baada ya kushauriana wakapendekeza kwa watu wa familia ya marehemu Dkt. Leitner ya kwamba kwa kuwa Idara hiyo na majengo yaliyoihusu pamwe na Shah Jahan Mosque na Sir Salar Jang Memorial House, vilijengwa na kuanzishwa kwa fedha za Waislamu, basi hivyo kwa kweli ni mali ya ushirika ambayo yapaswa kusimamiwa na kutawaliwa kama mali ya watu, na Waislamu au kwa niaba ya Waislamu.



Sir Muhammad Zafrullah Khan r.a. - Mtunzi wa kitabu hiki

Hilo halikukubaliwa na familia ya Leitner, waliodai mali yote kuwa yao binafsi. Jambo hilo likakabidhiwa kwa wanasheria, na baada ya kushauriana kirefu ikakubuliwa kwamba msikiti na Memorial House na eneo la kuzunguka wakabidhiwe Waislamu, na wakina Leitner wanaweza kubakiwa na Idara pamoja na eneo kubwa linalohusikana nayo. Hapo ndipo Khwaja Kamaludddin akaonana na Mheshimiwa Seyyid Amir Ali na kupendekeza kwamba Shah Jahan Mosque na Memorial House aweza kukabidhiwa yeye; hapo atakaa katika Memorial House na atasimamia sala tano za kila siku zisaliwe kama kawaida. Seyyid Amir Ali akashauriana na Mirza Abbas Ali Beig na Waislamu wengine katika London, na pendekezo la Khwaja Sahib likakubaliwa. Ushirika wa Msikiti wa Woking ukafanywa na Bwana Khwaja akaenda kukaa katika Memorial House na kushika usimamizi wa msikiti, lakini sala ya Ijumaa ikasaliwa katika ukumbi fulani uliopangwa kwa shabaha hiyo huko Notting Hill Gate, London, na sala ya Ijumaa ikaongozwa na Khwaja Kamaluddin, aliyewasili kutoka Woking kwa shughuli hiyo.

Wajibu wake kuhusu usimamizi wa msikiti na kutoa jarida la *Islamic Review* ikawa kazi ambayo Bwana Khwaja akaona shida kutekeleza ipasavyo akiwa peke yake. Akamwomba Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. msaada, ambaye akamtuma Chauhdri Fateh Muhammad Sial r.a., M.A., kijana Mwahmadiyya mwaminifu aliyejitolea mhanga, mnamo kiangazi cha mwaka 1913, ili kumsaidia. Bwana Khwaja akafanya mpango kwamba Sheikh Nur Ahmad, mtu mwema sana lakini mzee kidogo, aliyekuwa karani wake kwa kazi ya uwakili katika Lahore, aweze kusafiri pamoja na Bwana Sial r.a., ili kuangalia mambo ya Bwana Khwaja ya binafsi.

Maisha yangu huko Uingereza yaliendelea vizuri. Ombi moja aliloniagiza Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. kuomba lilikuwa: Mola, nijalie rafiki mwema. Hilo likaleta tunda katika muda wa wiki nane baada ya mimi kuwasili London. Kwa bahati njema nikapata kuonana na mwanafunzi mmoja Mjerumani mwenye umri kama mimi aliyewasili London kwa masomo ya uhandisi na akaingia katika King's College, ambako mimi niliingia kwa ajili ya masomo ya Sheria. Huyo bwana alitokana na familia ya ukoo wa waungwana wa Pomerania. Babake alikuwa mjumbe wa serikali lakini sasa alikuwa amestaafu na akawa anaishi Brussels ambako alikuwa na shughuli kubwa za viwanda. Mamake alikuwa Mfaransa. Upesi tukawa marafiki sana; akathibitika kuwa ndugu kweli kwangu. Ndiye yule rafiki Mjerumani aliyetajwa mwishoni mwa barua ya Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. ya Septemba 16, 1913. Urafiki wetu ukadumu maisha yake mazima. Alipigana upande wa Ujerumani katika Vita Vikuu Vya Kwanza, alijeruhiwa mara mbili, alipata nishani ya Iron Cross na akafanywa Knight of Hohenzollern. Baada ya vita tukaanza tena kuandikiana. Alipoteza kila kitu lakini akaendelea kishujaa. Akaenda Uingereza mnamo 1924 na akakaa London. Mara nyingi tulipata kuonana London, naye akatutembelea mara nyingi huko India.

Pindi nilipokuwa Uingereza kama mwanafunzi, barua za Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. zilikuwa chanzo cha kunifariji sana na kunichangamsha mno. Mara nyingi nilihisi kusaidiwa kidhahiri kwa sababu ya yeye kuniombea. Mwanzoni mwa Machi 1914 nikapata idhini yake ya kwenda bara katika likizo za Pasaka. Kabla sijaondoka habari ya kuhuzunisha sana ya kifo chake ikapokelewa kwa njia ya Khwaja Kamaluddin. Nilipomwendea kwa maelezo akaniambia:

"Hali yenyewe ni ya kutia wasiwasi. Sijui sana. Nimepokea simu tatu fupi sana za maandishi. Ya kwanza iliarifu kufariki kwa Maulawii Sahib. Ya pili ikasema kwamba Mian Mahmud ametangazwa kuwa *Khalifa*. Ya tatu ikasema kwamba kulitokea mafarakano na waliotengana wakaitwa waasi. Sielewi nisemeje kwa hayo yote!"

Siku hizo barua kutoka Panjab zilikuwa zinawasili London baada ya siku kumi na tano. Nikafadhaika sana, na nikafahamu kikamilifu lakini ikashindikana kufanya chochote. Nikaenda likizo zangu kwa moyo wa kusumbuka na mashaka, lakini kwa kufanya maombi. Niliporudi baada ya wiki tatu nikakuta barua chunguchungu zaningojea. Barua ya mama yangu ikasema ya kwamba Jumuiya imepatwa na msiba mkubwa sana. Kulitokea mafarakano ya kusikitisha. Hadhrat Sahibzada Mirza Bashiruddin ndiye *Khalifa* wa haki. Mimi nimekwisha fanya baiati yake, nawe ufanye hivyo mara moja. Babangu akaandika kwamba hili ni swala linalohusu dhamiri, na kwamba yeye hataniagiza lolote. Napaswa kujiamulia mwenyewe baada ya kutafakari sana na kuomba dua kwa bidii kwa kupata mwongozo. Usomaji wa haraka wa barua zangu nyinginezo ukanihakikishia kwamba kiini cha hitilafu ni kuwepo au kutokuwepo kwa Imam wa kiroho wa Jumuiya mwenye madaraka ya juu kabisa. Kuhusu swala hilo moyo wangu ulikuwa mweupe; sikuwa na wasiwasi hata kidogo. Barua zilikuwa ziende jioni hiyo hiyo. Nikashika kalamu na kumwandikia Hadhrat Khalifatul Masihi wa pili barua ya kufanya baiati. Pia nikaandika nyumbani kuwaarifu wazazi wangu habari hiyo.

Itaendelea toleo lijalo, Inshallah

'AHMADIYYA SECONDARY SCHOOL KITONGA' - YAPATA USAJILI RASMI

Kwa fadhili kuu za Mwenyezi Mungu Shule yetu ya **'Ahmadiyya Secondary School Kitonga'** imesajiliwa rasmi na Wizara ya Elimu na mafunzo ya ufundi.

Alhamdulillah thumma Alhamdulillah

Shule imepatiwa Usajili Na. S. 4681

Tunamuomba Mwenyezi Mungu Aijaalie shule hiyo iwe ni chemchem ya kweli ya elimu na maarifa na Aifanye kuwa ishara ya baraka zake juu yetu. Amin.

Islam sio Dini ya vurugu, bali ni Dini ya amani, subira na maelewano

Na Mwl. Kaisi Ali - Mkongotema, Songea (0714920017)

Kwao wao wamelitafsiri neno Jihad ni kupambana na mtu yeyote mpinzani asiyekuwa Mwislam na hata ikibidi ni lazima auawe huyo mpinzani. Kwa hakika kuamini hivyo ni ujinga na hiyo ni tafsiri mbovu kabisa ya neno Jihad, kwa sababu vita vya Jihad alivyopigana Mtukufu Mtume Muhammad (saw) vilikuwa ni vita vya kujitetea ambapo makafiri wa Maka walitaka kumwua yeye pamoja na wafuasi wake (Masahaba zake).

Makafiri wa Maka walionesha dhuluma ya hali ya juu kwa Mtukufu Mtume Muhammad (saw) pamoja na wafuasi wake hata ikalazimika baadhi ya wafuasi wake walihama Maka wakaelekea uhamishoni katika nchi ya Uhabeshi ambayo ni (Ethiopia ya leo) na Mtume Muhammad (saw) alihama Maka akaenda Madina.

Haya yote yalifanyika ili kuwakimbia maadui zake waliotaka kuwaangamiza Waislam, hata hivyo makafiri wa Maka hawakutosheka bali waliamua kumfuata Mtukufu Mtume (saw) kule kule uhamishoni Madina kwa nia ya kutaka kumwua yeye mwenyewe Mtume (saw) pamoja na Masahaba zake. Na ifahamike kwamba Mtume (saw) baada ya kupewa utume alikaa Maka kwa muda wa miaka 13.

Kwa muda wote huo maadui zake yaani Makafiri wa Maka waliendelea kumfanyia mateso Mtukufu Mtume (saw) pamoja na wafuasi wake lakini Mtume (saw) pamoja na wafuasi wake waliendelea kuwa na subira na uvumilivu wa hali ya juu sana, hawakuweza kuleta vurugu za aina yoyote ile mpaka Mtukufu Mtume (saw) alipopata amri kutoka kwa Mwenyezi Mungu ya kutakiwa kuhama katika mji wa Maka aelekee Madina uhamishoni.

Makafiri wa Maka hawakutosheka na utesaji ule wakaamua kumfuata kule kule Madina kwa nia ya kutaka kuendelea kumtesa yeye na wafuasi wake hatimaye watimize adhma yao ya kutaka kumwua, na kutaka kuifuta dini tukufu ya Kiislamu. Mwenyezi Mungu baada ya kuona nia hii ya makafiri wa Maka ya kutaka kumwua Mtume wake ndipo Alipomuamuru Mtume (saw) kwamba sasa inabidi awajibu wapinzani wake na Mwenyezi Mungu Mwenyewe Akaahidi kwamba Atamsaidia. Hivi ndivyo vita alivyopigana Mtukufu Mtume (saw).

Alipigana vita vya Jihad kwa ajili ya kujitetea dhidi ya wapinzani wake waliotaka kumwangamiza yeye pamoja na wafuasi wake. Pengine niseme kwamba kundi kubwa la waumini wa dini tukufu ya Kiislam hawana ufahamu wa kutosha kuhusiana na mafundisho ya dini tukufu ya Kiislam, wengi wao wanafuata mkumbo hivyo mara nyingi wanadanganywa na masheikh wao wanaotafuta vyeo na maslahi yao binafsi ya kutaka maisha ya kidunia, wanawahamasisha na kuwarubuni wafuasi wao wafanye fujo na maandamano eti wakisema kwamba wanadai haki za Waislam.

Na wakati wanafanya hayo maandano wanakuwa wamejificha na kuwatelekeza wafuasi wao wakila kichapo na kisago kutoka kwa vijana wetu askari Polisi waliosomea kuwatuliza watu wenye kufanya fujo. Kwa Waislam mambo hayo ya vurugu wanayoyafanya ni mambo yaliyo tabiriwa na Mtukufu Mtume Muhammad (saw);

"Imesimuliwa na Hadhrat Ali (ra) ya kwamba Mjumbe wa Allah (saw) alisema (kwamba) ni karibu iwadie juu ya watu (Waislam) zama ambazo hakitabaki chochote cha Islam isipokuwa jina lake, wala hakitabaki chochote cha Qur'an isipokuwa maandishi yake (Katika zama hizo) Misikiti yao itaendewa (kidhahiri) na watu wengi lakini itakuwa (ni misikiti) mitupu bila mwongozo, Maulamaa wao (yaani Masheikh wao) watakuwa wabaya sana kuliko (watu) wowote waliochini ya mbingu. Na kutoka kwao (hao Masheikh wao) watazusha fitina na fitina hiyo itawarejea wenyewe" (Mishkatul Kanzul Umal).

Na pia Mtukufu Mtume Muhammad (saw) alisema kwamba;

"Zitatokea juu ya umati wangu (Waislam) zama za fadhaa na ndipo watu (Waislam) watawaendea Maulamaa (Masheikh) wao (kusaidiwa) lakini watawakuta kumbe ni manyani na nguruwe. (Yaani hawatakuwa na elimu mzuri ya kiroho)" (Kanzul Umal).

Ndugu zangu wasomaji wapendwa usemi huo hapo juu wa Mtukufu Mtume (saw) kwa ajili ya Waislam hivi sasa umeshatimia hakuhitaji kuangalia kwa darubini kali, Waislam wengi hivi leo ni wa majina tu sio Waislam wa kufuata mafundisho ya Qur'an Tukufu.

Hivi sasa katika miskiti yao kumejaa na majungu na fitina, badala ya kufanya ibada Masheikh wao ndio vinara wa kuandaa majungu na fitina hizo na pia ifahamike kwamba zama hizi ni zama za mwisho ambapo Manabii mbalimbali waliopita walitoa utabiri kuhusiana na wakati huu tulionao, ya kwamba katika zama hizi dunia itachafuka kwa maovu mengi sana kiasi ambacho amani itatoweka na binadamu watafanya maovu ya aina mbalimbali.

Kama inavyosemwa katika Biblia kwamba;

"Hata alipokuwa ameketi katika mlima wa mizeituni, wanafunzi wake wakamwendea kwa faragha, wakisema, tuambie mambo hayo yatakuwa lini? Nayo ni nini dalili yake ya kuwako, na ya mwisho wa dunia? Yesu akajibu akawaambia, angalieni, mtu asiwadanganyeni, kwa sababu wengi watakuja kwa jina langu, wakisema, mimi ni Kristo nao watadanganya wengi.

Nanyi mtasikia habari za vita na matetesi ya vita, angalieni msitishwe, maana hayo hayana budi kutokea, lakini ule mwisho bado. Kwa maana taifa litaondoka (kwenda) kupigana na taifa (jingine), na ufalme kupigana na ufalme, kutakuwa na njaa, na matetemeko ya nchi mahali mahali". (Math.24:3-7).

Utabiri huo hapo juu alioutoa Bw. Yesu Kristo unawahusu sana ndugu zangu Wakristo, utabiri huo hivi sasa umeshatimia tayari hakuna hata jambo moja



Mwl. Kais Ali

alilolitamka Bw. Yesu kwenye utabiri huo ambalo halijatimia. Kwa mantiki hiyo kutokana na hali hiyo ya machafuko ambayo Manabii mbalimbali waliopita waliitabiri. Pia Manabii hao hao walitabiri ujaji wa Mtu mkubwa sana (Nabii) hapa Duniani atakayekuja kuwasaidia wanadamu na matatizo watakayo kuwa nayo katika zama hizo na kuusuluhisha ulimwengu kutokana na maovu, fitina, vurugu na fujo zote ili amani itawale.

Kwa Waislam waliambiwa na Mtukufu Mtume Muhammad (saw) kwamba atawafikieni Imam Mahdi ambaye ni Nabii Isa kwa namna ya mfano yaani atazaliwa mtu mwingine hapa hapa duniani ambaye atafanana sana kimajukumu, khulka na tabia, na Nabii Isa yule, wa mara ya kwanza ambaye alikuja kufanya kazi kubwa sana ya kuwarudisha wana wa Israeli ndani ya mafundisho ya Torati ya Mussa (as).

Na ndivyo ilivyotabiriwa na Mtukufu Mtume Muhammad (saw) kwamba huyo Imam Mahdi ambaye ni Nabii Isa wa Waislam atakuja kufanya kazi kubwa ya kuwasuluhisha Waislam waachane na itikadi mbovu za kufanya vurugu na fujo na maovu yote. Wayafuate mafundisho safi ya Qur'an Tukufu.

Na kwa upande wa ndugu zetu Wakristo wameambiwa katika Injili ya kwamba Bw. Yesu Kristo atafika mara ya pili, ukweli ni kwamba Yesu yule wa Nazareti aliyezaliwa na mama Mariam hatafika tena hapa duniani kwani sio mpango wa Mwenyezi Mungu kuwaleta Manabii waliokwisha pita zamani wao wameshafariki tayari hata Bw. Yesu Kristo ameshafariki tayari na kaburi lake lipo nchini India katika jimbo la Kashmir mtaa wa Khanyar Srinagar.

Hivyo basi ilivyotabiriwa kufika kwa Yesu mara ya pili maana yake ni kuzaliwa kwa mtu mwingine katika dunia hii ambaye atafanana sana kimajukumu, kikhulka na kitabia kama vile alivyo kuwa Bw. Yesu Kristo wa Nazareti, kwa mfano huo Bw. Yesu Kristo aliwaeleza Mayahudi waliokuwa wanamsubiri Nabii Eliya ashuke kutoka mbinguni, yeye Yesu akawaambia kwamba Yohana mbatizaji ndiye Eliya na mwenye masikio na asikie. (Matayo11:13-15) na Math.17:10-13).

Hivyo basi kama vile alivyokuja Eliya katika dhati ya Yohana Mbatizaji ndivyo alivyokuja Bw. Yesu Kristo katika dhati ya mtu mwingine. Hivyo basi ndugu zangu wapendwa Waislam na Wakristo napenda kuwaeleza kwamba hivi sasa la mgambo limelia toka mbinguni kwamba aliyekuwa anasubiriwa kufika zama hizi kwa Waislam na Wakristo tayari ameshafika ni Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad (as) ambaye kwa amri ya Mwenyezi Mungu ameanzisha Jumuiyya ya Waislam ya Ahmadiyya, yeye ndiye Nabii aliyetimiza utabiri wa kufika mara ya pili kwa Nabii Isa (as) na Yesu Kristo kwa Waislam na Wakristo, yeye amekuja kufanya kazi ile ile ya Manabii waliopita, amekuja kufundisha wanadamu khulka na tabia njema. Kwani ifahamike kwamba anayeweza kuwabadilisha wanadamu tabia si mwingine bali kazi hiyo anayekabidhiwa ni Nabii wa Mwenyezi Mungu, hivyo basi hivi sasa duniani kote wanadamu wakitaka amani na utulivu ipatikane basi wanatakiwa wamfuate Nabii huyu wa Mwenyezi Mungu aliyetumwa katika zama hizi, yaani Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad (as).

Yeye ameleta mafundisho safi kabisa, yatakayoleta amani na utulivu duniani kote mfano wake unaonekana kutoka kwa wafuasi wake yaani Wa Ahmadiyya ambao wamesambaa duniani kote wao ni watu wa amani hata Serikali zote duniani wanafahamu hivyo kwamba wa Ahmadiyya ni watu wa amani na hawajajihusisha na fujo za aina yoyote na wala hawajawahi kufanya maandamano mahala popote duniani. Hii ni kutokana na kufuata mafundisho safi aliyokuja nayo huyu Nabii wa Mwenyezi Mungu.

Kabla sijamaliza makala yangu napenda kunukuu maneno ya Mwanzilishi Mtukufu wa Jumuiyya hii ya Waislam ya Ahmadiyya, yeye alisema kwamba;

"Kwa wakati tulio nao, kwani imeandikwa ya kwamba wakati wa ujaji wa Masihi Aliyeahidiwa vita vya upanga na vya kidini vitakwisha".

"Ni dhahiri Masihi (atakapofika) hatatumia upanga ama silaha zozote za kidunia kwani silaha yake itakuwa maombi. Istiqama ndiyo itakuwa silaha yake. Ataweka jiwe la msingi la mapatano na kuwaleta pamoja wale wenye munkari na wapole. Zitakuwa ni zama za kuunganika pamoja huruma na mapenzi. Kwa hakika ninasema kweli.

Huu sio wakati wa Jihadi ya upanga, msimuasi Mtume Mtukufu Muhammad (saw) aliye ni Mtume wa Mwenyezi Mungu. Masihi tayari amekwishafika na tayari amekwisha toa fatwa. Kuweni mbali na silaha zinazotumika kumwaga damu. Kutoacha mauaji ya namna hii na kuhubiri dhana hizo za umwagaji damu sio mwenendo wa Islam.

Mtu anayenikubali mimi sio tu anaacha kuhubiri dhana hizo potofu bali ataziona kuwa dhana hizo kuwa ni uovu na zinazostahili laana ya Mwenyezi Mungu".

Pia Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad (as) alisema kwamba;

"Kwa wale wafuasi wangu ambao wanaamini katika ujumbe wangu, ninawaomba wawe mbali kabisa na uchafu wote huo (wa Jihadi ya kumwaga damu za binadamu bila sababu).

Mwenyezi Mungu Amenituma katika nyoyo za Masihi Mwana wa Mariam na kunifanya Masihi Aliyeahidiwa. Hivyo ninatangaza muwe mbali na uovu na muwe na huruma na binadamu. Safisheni nyoyo zenu na husuda na temeni sumu chafu na mtakuwa kama malaika. Ni imani ya hovyo mno ambayo haina huruma na mapenzi kwa binadamu. Ni njia mbaya mno iliyojaa miiba n a ubinafsi.

Enyi nyinyi mliopamoja nami jivueni na uchafu huo, tafakarini sana juu ya jambo hili. Nini hasa shabaha ya dini? Je ni kuwatesa watu wengine?. Hapana, dini ni njia inayomuelekeza mtu kwa Mwenyezi Mungu. Mtu hawezi kumfikia Mwenyezi Mungu na wala hakuna ambaye amewahi kufanikiwa hadi amefanikiwa kuzielewa sifa za Mwenyezi Mungu. Tafadhalini sana kuweni wenye huruma kabisa kwa kila mtu, nifuateni mimi na nitawaonyesha njia mtakapopata imani ya kweli itakayowafanya muwashinde watu wengine.

Achaneni na roho mbaya na muwe mbali sana na mambo ya wivu. Muwe na huruma kubwa sana kwa binadamu na muwe karibu sana na Mwenyezi Mungu. Safisheni nafsi zenu. Ni kwa njia hii miujiza itaanza kutokea. Sala zako zitapokelewa na malaika watateremka kutoka mbinguni ili kukusaidia. Hii si kazi ya siku moja, anza kupiga hatua na nenda mbele. Nimekuja kwenu na amri, sasa ni mwisho wa Jihad kwa kutumia upanga, lakini Jihad ya kusafisha nafsi zenu inaendelea.

Na hili jambo sio kwamba nimelibuni, haya ni mapenzi ya Mwenyezi Mungu. Jikumbusheni Hadithi ya Mtukufu Mtume (saw) iliyomo katika Sahihi Bukhari ambapo pameandikwa katika mnasaba wa Masihi Aliyeahidiwa (YADA-UL-HARB) - yaani Masihi Aliyeahidiwa atakomesha (Jihadi) mapigano yote ya kidini.

Hivyo nawaamuru wote ambao ni wafuasi wangu kujiweka mbali na dhana za namna hiyo. Safisheni nafsi zenu na shindaneni katika usafi wa mioyo na kuonyesha huruma kwa walio dhaifu. Enezeni amani duniani na imani yetu itashamiri"

Ndugu zangu wasomaji wapendwa maneno yaliyopo hapo juu ni ujumbe tosha kwa watafutao na wapenda amani duniani. Haya ni maneno ya mtu aliyetumwa na Mwenyezi Mungu ili aje kuusuluhisha ulimwengu kutokana na maovu. Hivyo basi yule ndugu yangu anayetaka amani ya kweli na kuutafuta ukweli wa mafundisho safi basi namkaribisha katika Jumuiyya hii ya Waislam ya Ahmadiyya ambayo imeanzishwa na Nabii wa Mwenyezi Mungu aliyetumwa katika zama hizi za upotevu kuja kuwakomboa wanadamu kutokana na maovu. Hivyo ndugu yangu usichelewe fanya haraka sana kuja kupanda Safina hii ili uokolewe na matatizo ya zama hizi.

Kwani Masihi mwenyewe wa zama hizi alisema kwamba;

"Nikimbilieni sasa, kwani bado upo wakati, yule mtu anayenikimbilia hivi sasa, namfananisha na yule ambaye amepanda Jahazi wakati hasa wa tufani, lakini mtu asiyeniamini naona anajitupa mwenyewe katika tufani na hana chochote cha kujilinda nacho. Mwombezi wa kweli ni mimi niliye kivuli cha yule mwombezi mkuu".

-Mwisho-

Mpango wa Waqfu Nau: Sifa ya pekee ya Ahmadiyya

Kutoka uk. 11

neema hiyo ambayo Mwenyezi Mungu Ametupatia leo.

Pia yafaa kukumbukwa kwamba, bila ya maombi, maombi yaliyojaa jadhba ya kweli na huruma, hatuwezi kuyapata makusudio yetu. Hivyo mambo haya, na mawazo haya, yanapaswa yawemo kwa aliyejitolea wakfu au wakfe nau kikwelikweli. Bila ya hayo kutarajia mafanikio ni ndoto tu. Bila ya mambo haya inakuwa ni nembo tu ya wakfu au ya wakfe nau aliyoivaa, kunakuwa hakuna chochote zaidi ya hapo. Makusudio yetu sio tu kuchukua nembo wala hayakuwa makusudio ya wazazi wale waliowatoa watoto wao katika Kurbani hii.

Hivyo kama nilivyosema, kwa ajili ya wazazi na pia kwa ajili ya waakifine nau, ni muhimu kwamba myatekeleze majukumu yenu. Mimi nataka tena kuelekeza kwamba ili kueneza dini duniani, elimu ya dini ni muhimu, na elimu hii yaweza kupatikana zaidi katika idara ile ambayo makusudio yake ni kufundisha tu dini, na idara hii ndani ya Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya inafahamika kama Jamia Ahmadiyya.

Leo, kwa fadhili za Allah, kama nilivyosema, kwamba Jamia hazipo tu Qadian au Pakistan, hazikuishia huko tu, bali ipo pia Uingereza, ipo pia Ujerumani, ipo pia Indonesia, ipo pia Canada, na ipo pia Ghana. Kama nilivyosema, kwa ajili ya kutoa mafunzo ya Shahid, Jamia imefunguliwa huko Ghana. Kwanza ilikuwepo Jamia lakini ilikuwa ni kwa ajili ya kutoa tu waalimu kwa kozi ya miaka mitatu. Hivyo hii Jamia Ahmadiyya iliyofunguliwa huko Ghana, hiyo itatoa Masheikh wa daraja la Shahid kwa ajili ya Afrika yote. Halikadhalika kuna Jamia Ahmadiyya huko Bangladesh.

Kazi ya Tabligh (mahubiri) ni kazi iliyopanuka sana, na hii inaweza ikategemewa zaidi kwa Wabashiri waliofunzwa kwa utaratibu. Hivyo idadi kubwa zaidi ya waakifiine nau inapaswa wajiunge na Jamia Ahmadiyya, wakati kutokana na takwimu ambazo nimezieleza, katika kila nchi hatutaweza kwa wakati ujao wa karibu au hata wa mbali kuweka Mbashiri kila mahali na hadi wakati huo waalimu na wabashiri hawatakuwepo kikamilifu, itakuwa vigumu sana kutekeleza mipango ya kimapinduzi ya kimahubiri. Ile taarifa iliyokuja toka kwenye kitengo husika (ambayo ni taarifa ya hadi mwaka 2012) ni kwamba kwa wakati huu duniani kote idadi ya waakifine na waakifaate nau wenye umri wa zaidi ya miaka kumi na tano ni elfu ishirini na tano, ambapo wanaume ni elfu kumi na sita mia tisa na themanini na nane, na miongoni mwao, waakifine nau wa Pakistan ni elfu kumi mia sita themanini na saba.

Baada ya Pakistan ni Ujerumani kwenye waakifine nau zaidi, wavulana elfu moja mia nane sitini na saba na mabinti elfu moja mia moja hamsini na tano. Halafu Uingereza wavulana mia tisa kumi na nane, idadi yao kamili ni mia saba hamsini na nane na waliobakia ni kama wasichana mia nane hivi.

Lakini idadi ya wanaokuja Jamia Ahmadiyya ni ndogo sana, Ujerumani na pia Uingereza. Ndani ya Jamia zote hizi mbili wanafunzi huja kutoka hata katika nchi zingine za Ulaya, kwa namna hii idadi hii inazidi kupungua. Halikadhalika idadi ni ndogo kwenye Jamia za Marekani na Canada. Jumuiya huwa zinaomba zipatiwe Wabashiri, basi muwe tayari kuwatoa watoto wa waakifiine nau kwa ajili ya Jamia. Kwa sasa Canada na Marekani kuna takriban wakifiine nau mia nane walio na umri wa zaidi ya miaka kumi na tano. Kama watayarishwe ndani ya miaka miwili ijayo idadi ya watakaoingia kwenye Jamia inaweza kuongezeka maradufu.

Sio kwa ajili tu ya kuwa Murabbi au Muballigh, bali baada ya kusoma Jamia na kupata elimu ya dini wanaweza pia kutafsiri vitabu vya Masihi Aliyeahidiwa a.s. katika lugha zao. Wanaweza pia kuchukua masomo makhsus ya kujifunza lugha mbali mbali baada ya kusoma Jamia. Halafu wale ambao hawaji Jamia, basi waelekee katika kujifunza lugha mbali mbali. Na hao wenye kujifunza lugha, kwa uchache, kama vile Hadhrat Khalifatul Masih wa nne rh.a. pia alivyosema, na ni muhimu pia kuwa azifahamu angalau lugha nne, mojawapo ikiwa ni lugha yake mwenyewe, ya pili Kiurdu na ya tatu Kiarabu. Asipojifunza Kiarabu, basi kuisoma Qur'an na kufahamu maelezo ya Qur'an Tukufu na katika kutafsiri, kama hafahamu Kiarabu sawasawa basi hata tafsiri ya Qur'an Tukufu haiwezi kufanyika sawa sawa.

Na kusoma na kujifunza Kiurdu ni muhimu kwa sababu hii kwamba uelewa sawasawa wa dini kwa wakati huu unaweza kupatikana kwa usomaji wa vitabu vya Masihi Aliyeahidiwa a.s., kwa sababu, maelezo yake, vitabu vyake na maandiko yake ndiyo hazina za nuru ambazo zaweza kuleta mapinduzi duniani kwa kuweza kuieleza dunia mafundisho sahihi ya Islam, ambazo zaweza kuifahamisha dunia maelezo sahihi ya Qur'an Tukufu.

Hivyo bila ya kujifunza lugha ya Kiurdu huwezi kupata umahiri katika medani za lugha. Kulikuwa na wakati ambapo kulikuwa na shida sana ndani ya Jumuiya ya tafsiri, hata sasa bado kuna shida, lakini sasa kwa kiwango fulani, wale watoto wasomao Jamia katika nchi mbali mbali, shida hii yaenda ikipungua, makala za Jamia Ahmadiyya zinatafsiriwa Kiurdu, vitabu vya Masihi Aliyeahidiwa a.s., baadhi ya vitabu vya Hadhrat Khalifatul Masih wa pili r.a. vimetafsiriwa na sawa na maelezo ya wasimamizi wa wanafunzi, vimetoka vizuri. Lakini kwa vyovyote vile, hata kama viwango visiwe vya juu sana, vinaweza vikaboreshwa lakini hata hivyo jitihada imeshafanyika.

Lakini hawa ni wanafunzi wachache tu wanaopewa vitabu. Sisi twahitaji mabingwa wa lugha wengi kadiri iwezekanavyo, kwa namna hii waakifiine nau wanapaswa kuelekea upande huu Kama kuna yeyote anayepata umahiri katika lugha fulani mbali na wanafunzi wa Jamia, basi huyo, kama nilivyosema, aelekee katika kujifunza Kiarabu na Kiurdu, mbali na hayo makusudio, hayo hayawezi kufanikiwa, kwa ajili hiyo lugha inapaswa ielekewe sana.

Baadhi ya watu wanaishutumu Jamia Ahmadiyya kwamba hapa hakuna mafundisho mazuri, hapa au Ujerumani au sehemu fulani. Hii ni shutuma ya hovyo kabisa. Shutuma yao ni kwamba hawa wanaomaliza Jamia hawawezi hata kidogo kuongea Kiarabu, au hawakiongei vizuri. Kuhusiana na suala la umahiri katika lugha, kwa kuwa masomo mbali mbali hufundishwa hapo Jamia Ahmadiyya, hivyo hawalielekei somo moja pekee. Kwenye vyuo vingine vikuu na vile vya kidini kama somo hilo lafundishwa basi ni somo moja tu hufundishwa na mtu anaweza akalisoma vema, lakini hapa masomo mengi tofauti hufundishwa, ila kama inaonekana kwamba mwanafunzi fulani ana mwelekeo mzuri kwenye lugha fulani au ana mwelekeo mzuri wa kujifunza lugha, basi huyo, Inshaallah, atapelekwa kwenye kozi makhsus ya lugha. Na halafu manung'uniko hayo kuhusiana na uongeaji wa lugha ya Kiarabu, nayo pia yataondoka.

Lakini kwa vyovyote vile, kuhusiana na mafundisho, elimu hiyo itolewayo ni elimu pana sana ambayo, kwa fadhili za Allah, wanafunzi wa Jamia wanaipata. Pakistan kwa kuwa zimekuwa ni Jamia za zamani, huko hupelekwa pia kwenye kozi makhsus za (ku specialize) kuspeshalaiz. Nimepata taarifa za ujerumani za baadhi ya watu za kisingizio cha kutopeleka watoto Jamia. Kama nilivyosema kuwa wale wanafunzi waliomaliza Jamia Uingereza na Canada kwa uzoefu mdogo walioupata wanatoa athari nzuri sana kwenye uwanja wa mahubiri. Na elimu hii, kama nilivyosema itaendelea kukua, hatua kwa hatua. Hivyo wale watu wasemao maneno haya, wenye kuwakatisha tamaa baadhi ya watoto wanaotaka kuingia Jamia, watu hao ni wenye fitna tu au unafiki, hivyo wao pia wanapaswa kuomba istighfar.

Kitengo hicho cha Wakfe Nau kimetoa baadhi ya mambo ya kiutendaji yapasayo kuelezwa ambayo ninayarudia, huenda hapo mwanzo nilishayaeleza. Katika wakfe nau, watoto wafikapo umri wa balehe au kabla ya hapo wazazi wawape watoto malezi ya kujifahamu kuwa wazazi wao wamewatoa wakfu, haya nimeshayaeleza hapo awali. Na katika kila hatua ya elimu umuelekeze na halafu upate pia mwongozo toka kwenye ofisi ya Wakfe Nau. Watoto waulizwe kwamba wamefikia hatua gani na nini wafanye. Na kama watake kufanya watakavyo wenyewe au watake kuenda kwenye kitengo ambacho kwa sasa Jumuiya haina shida nayo, basi waombe ruhusa ya kujitoa kwenye wakfu.

Mabinti walio waakifaate Nau, wenye asili ya Pakistan, waliokuja toka Pakistan, wenye kuweza kuongea Kiurdu, wajifunze pia kusoma kiurdu, wale waishio hapa katika nchi za nje. Na pia wajifunze lugha za wenyeji, iwe Kiingereza au Kijerumani, au katika maeneo ambayo Kiingereza ndio lugha inayotumika kitaifa wakati lugha ya wenyeji ikiwa ni nyingine, hiyo pia mjifunze, Kiarabu pia mjifunze, halafu mjitolee kwa ajili ya kutafsiri. Nimeshuhudia kwamba wanawake na mabinti wana uwezo zaidi katika fani za lugha, hivyo wanaweza kujitolea.

Halafu kuna madaktari, waalimu, hawa mabinti pia wanaweza kujitolea baada ya kuwa madaktari na waalimu, vivyo hivyo wavulana pia. Inapaswa iwe hivi na kitengo kinapaswa kifahamu katika kila hatua.

Jamaat za maeneo husika, kwa ajili ya kuwaongoza wavulana na wasichana kwenye tarbiyyat (malezi), kwa uchache mara mbili kwa mwaka ambapo utaratibu wao unapaswa kufanywa ambamo mna mwongozo wa elimu na kazi.

Moja ya malalamiko toka kwenye ofisi hii ya wakfe nau ni kwamba baadhi ya wazazi baada ya kutoa wakfu, baada ya kupata namba ya wakfu, hukata kabisa mawasiliano na jamaat yake na Markaz, au wanakuwa hawana mawasiliano kama yanavyostahili kuwepo. Halafu baada ya kufika hatua fulani wakati ofisi inasema kwamba yapaswa atolewe maana hakuna mawasiliano yoyote, miaka minane hadi kumi imeshapita, wakati huo malalamiko huanza. Hivyo kupata namba ya hawala haina maana kwamba sasa mawasiliano yameshakatika na yeye ameshaingia wakfe nau. Ni muhimu kustawisha mawasiliano ya kudumu na ofisi ya wakfe nau na pia Katibu wa taifa wa idara hiyo na makao makuu pia.

Pia kuna Nisabu (ratiba ya masomo) ya waakifiine nau na waakifaate nau, mwanzoni ilikuwa tu ya msingi, sasa imeshafikia ya hadi umri wa miaka ishirini na moja. Hiyo pia inapaswa kusomwa na kushiriki kikamilifu kama mtihani utatolewa. Na juu ya hapo, kwa wavulana na wasichana wasome tafsiri na maelezo ya Qur'an Tukufu, wajuao Kiurdu waisome ya Kiurdu na wajuao Kiingereza wazisome zile Tafsiri kubwa tano za Kiingereza, Vitabu vya Masihi Aliyeahidiwa a.s. vilivyokwishatafsiriwa katika lugha mbali mbali wavisome kwa lugha wazifahamuzo, wadumu kuzisikiliza hotuba, waendelee kuongeza elimu zao, hii pia ni muhimu kwa ajili yao na halafu watume taarifa zake.

Makatibu wa wakfe nau katika baadhi ya sehemu si watendaji wa kazi, wamekalia tu madaraka kuna haja pia ya watu hawa kuwa watendaji wa kazi. Chaguzi zinakuja basi taarifa zinapaswa zifike kwamba ni makatibu gani wa wakfe nau ambao si watendaji wa kazi, na kama si watendaji wa kazi, hata kama watapata kura nyingi hawatateuliwa.

Nisab (ratiba ya masomo) imekuja hapo mwanzoni, kuna nisabu pia ya Jumuiya imetengenezwa na pale ambapo hakuna mpango wa kuweza kuwa na mipango tofauti, basi wakfe nau wanaweza kushiriki katika nisabu hiyo hiyo ya Jumuiya, ina tofauti kidogo tu. Sasa kama kutakuwa na mawasiliano kidogo tu ya pande mbili basi wale wenye umri wa atfal wanaweza kuisoma ile ya atfal na wale wenye umri wa Khuddam wanaweza kuisoma ile ya Khuddam, waliomo ndani ya Lajna wanaweza kuisoma ile ya Lajna au nisabu yaweza kuunganishwa kati yao.

Sasa kama chini ya nidhamu ya Jumuiya, Katibu wa Tarbiyyat (malezi), Katibu wa Taalim na Katibu wa Wakfe Nau wanafanya kazi chini ya vitengo vya Jumuiya, ni kazi ya Maamiri na Maraisi kuwakusanya. Tengenezeni utaratibu wa aina hii kwamba nisabu hii isomwe na hasa kuwajumuisha waakifiine nau. Halafu hiyo nisabu ya Wakfe Nau inaweza pia kuchapishwa kwa lugha za nchi mbali mbali. Sweden imeshachapisha katika lugha yake. Watu wa Mauricius wa huko Ufaransa wajitahidi kuichapisha kwa lugha ya kifaransa kwa ajili ya Ufaransa. Na jitihada hiyo isiwe ya kutamka kwa ulimi bali mnipatie taarifa ndani ya miezi miwili, bali mnipe taarifa hii mara moja kwamba nani awezaye kuitafsiri na tafsiri hii inatakiwa iwe tayari ndani ya miezi miwili.

Kujisomea kwa waakifiine nau kuwe hivi kwamba kila siku kuwe na kitabu cha kidini wajisomeacho hata kama wasome kurasa mbili tu, na kitabu cha Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa a.s. kama nilivyosema, ni bora zaidi wakisome hicho. Halafu Hotuba mbali mbali, asilimia mia ya waakifiine na waakifaat nau wazisikilize hotuba. Siku moja nilifanya utafiti hapa Uingereza darasani ambapo nikagundua kuwa ni asilimia kumi tu ndio husikiliza hotuba kwa kawaida. Muuelekee upande huu, wazazi na pia shuba ya Wakfe nau na hata waakifiine nau wenyewe pia. Uongozi unatakiwa kuwa waandaapo vipindi hivi vya waakife nau viwe vyenye kuvutia ambapo huelekewa kwa makini.

Halikadhalika uongozi wa kila nchi uunde kamati ifanye utafiti ndani ya muda wa miezi mitatu kwamba mahitajio ya nchi hizo kwa miaka kumi ni yepi, wanahitaji Wabashiri wangapi, wanahitaji watafsiri wa lugha wangapi, wanahitaji madaktari wangapi, wanahitaji waalimu wangapi pale penye mahitajio, na halikadhalika kama wanahitaji wataalamu mbali mbali ni wepi hao, wanahitaji wataalamu wangapi wa lugha za kienyeji, basi wafanye utafiti huu na wanapaswa watoe taarifa ndani ya miezi mitatu na shuba ya wakfe nau iifuatilie ipasavyo.

Baadhi ya watu wanataka kwenda kwenye biashara au wanataka kwenda kwenye jeshi la Polisi, au jeshini n.k. bila shaka waende huko, lakini watoe taarifa ya kujitoa kwenye wakfu.

Halikadhalika katika kila nchi kunapaswa kuwepo na kamati ya kutoa ushauri kwa waakifiine nau juu ya ajira zao itakayokuwa ikifuatilia kwa makini na kutoa taarifa Makao Makuu, au wale wenye kutamani kwenda kwenye ajira tofauti zipatikane taarifa zao halafu Markaz ifanye uamuzi wa kumruhusu katika sura gani.

Na halafu hii pia, kama ambavyo nimeshwahi kusema mara kadhaa, kwamba waakifiine nau wenye kufikisha umri wa miaka kumi na nane wasisahau kuijadidisha ahadi ya wakfe nau, wawe wakiandika na kutuma, waandike mkataba.

Halikadhalika kuna vijarida vimeanzishwa kwa ajili ya waakifiine nau, kwa wanaume kinaitwa Ismail na kwa wanawake kinaitwa Mariam. Hivi vinapaswa pia kutafsiriwa katika Kijerumani na Kifaransa. Kama kuna madhumuni yaliyoandikwa na wenyeji wa huko walio Waakifiine nau na Waakifaate nau yachapishwe, vinginevyo yanaweza kutolewa toka hapa na kuchapishwa katika lugha zao pamoja na Kiurdu na pia lugha za wenyeji.

Mwenyezi Mungu Awaelekeze wale wazazi wote waliowatoa watoto wao katika Wakfe Nau katika malezi na maombi kwa ajili ya watoto wao kwa namna hii kwamba wawe kweli wenye kustahiki kuwa wakfe nau, na watoto hao wawe kiburudisho cha macho kwa ajili ya wazazi wao.

Watoto nao pia wawe wenye kuwaelekeza wazazi wao kutimiza ahadi zao, Mwenyezi Mungu Awajaalie uwezo wa hayo na wajiunge kwa ukweli kabisa ndani ya kundi lile ambalo kazi yake ni kueneza tu dini, Mwenyezi Mungu Awajalie uwezo huo. Amin.

Mpango wa Waqfu Nau: Sifa ya pekee ya Ahmadiyya

Kutoka uk. 12

shauku ya kuifahamu dini na pia walioelekea katika kushikamana na maisha yao na pia pamoja na hayo ikazalika ari na jadhba ya kuihubiri Islam na kuwahudumia wanadamu.

Daima mkumbuke kwamba kaumu zilizo hai na Jumuiya zenye kupata maendeleo huwa hazikubali kuvunja ahadi ya hisia hizi, ya mawazo haya, ya jadhaba hizi na ahadi hizi. Kwa ajili ya kuzihuisha jadhba hizo daima huyatafakari mambo hayo. Kama uvivu ukitokea popote pale hufanywa utaratibu wa kuuondoa na jukumu la cheo cha ukhalifa ndilo hili hili kwamba, mara kwa mara kukumbushia maagizo ya Mwenyezi Mungu, ili kasi ya maendeleo ya Jumuiya isipungue kwa wakati wowote ule.

Kwa ajili ya kuueneza ujumbe wa Mwenyezi Mungu duniani, kundi moja liwe tayari baada ya lingine, kama vile mifereji inayodumu kutiririka huwa ni sababu ya kuirutubisha ardhi, halikadhalika kundi la kuitumikia dini, moja baada ya lingine, huwa linakuwa sababu ya kuirutubisha hali ya kiroho. Katika maeneo yale ambamo kilimo cha umwagiliaji kwa njia ya mifereji au visima hutumika, wamiliki wa ardhi wa huko wanafahamu kwamba kama kabla ya kumalizia kunyweshelezа shamba zima maji yakikatika, basi itabidi shamba zima lirudiwe kumwagiliwa maji yatakapopatikana, tena na hivyo wakati na maji pia hupotea bure.

Hivyo hivyo kama juhudi za kudumu hazitafanyika katika kazi za urekebishaji na uongozaji au wafanyao hizo juhudi wasiwepo, basi yale maji yafikayo bila kikomo, yaani ule ujumbe ufikao yaani ile jitihada ifanyikayo, huchelewa kunyweshelezа. Vikwazo huzalika katika kazi za Tabligh (Mahubiri) na Tarbiyyat (Malezi). Hivyo Mwenyezi Mungu Anasema kwamba katika kila kaumu liwepo kundi lililo tayari kutoruhusu ukatikaji wa mtiririko wa ufikishaji wa ujumbe wa Mwenyezi Mungu. Hivyo ndio sababu leo ninakumbushia jambo hili kwamba ule mfumo wa Wakf e Nau aliouanzisha Hadhrat Khalifatul Masih wa nne rh.a. kwa matarajio na maombi haya kwamba kila wakati liwepo kundi la kuitumikia dini. Mtiririko huu wa maji hautakatika asilan. Jumuiya itakuwa na watu wa kuyatafsiri maandiko ya Jamaat, waenezaji wa kazi za Mahubiri na malezi pia watapatikana kwa wingi, na kundi la waliojitoa wakfu wa kuendesha tandhim zingine za nidhamu ya Jumuiya pia wataendelea kupatikana. Hivyo, kuna haja ya kudumu kuliweka mbele yetu jambo hili.

Baada ya wazazi kuwatoa watoto wao, hawapaswi kutojiwajibisha na majukumu yao. Bila shaka jadhba ya kuwatoa watoto kwenye wakf e nau ni yenye kustahili kusifika. Kila mwaka huja maelfu ya maombi ya kuwatoa wakfu watoto katika wakf e nau. Lakini baada ya kuyatoa maombi hayo, majukumu ya wote, baba na mama, huongezeka. Kuwatayarisha watoto hao kwa makusudio haya makhsus, ambayo ni makusudio ya kuiokoa dunia na maangamio, kwanza kabisa juhudi za kujitayarisha namna hii ni za wazazi. Kuwaandalia watoto wakati wao kwa kuwaonyesha mfano kwanza kabisa ni lazima waunganishwe na Mwenyezi Mungu. Tangu utotoni, kwa ajili ya kuwaonyesha umuhimu wa Jumuiya na kuwa wenye kuwa tayari kwa ajili ya kila aina ya kujitolea, watoto wapewe tarbiyyat ya aina hii kwamba wasiwe wakiwazia kitu kingine chochote. Wafikapo katika umri wa kujitambua, wakati watoto wakishiriki katika mipangilio ya Jamaat na ya wakfe nau, basi ikithiri akilini mwao kwamba wao ni wa kujitoa tu kwa ajili ya dini. Hasa mjaze zaidi ndani ya akili za watoto kwamba: makusudio ya maisha yenu ni kupata elimu ya dini, kuna haja ya kujaza ndani ya akili za watoto wa wakfe nau jambo hili na kwamba ni lazima kwao kwenda kwenye idara zile za Jumuiya zifundishazo dini. Idadi ya watoto wa wakfe nau waendao kwenye Jamia Ahmadiyya (Chuo cha Wabashiri) inapaswa kuwa kubwa zaidi.

Lakini kuhusiana na idadi iliyopo mbele yangu, ukiacha Pakistan, idadi ya nchi zingine zote ni ndogo sana. Pakistan, kwa fadhili za Allah, wakati huu kuna wakifiine nau elfu moja na thelathini na tatu wanaosoma Jamia Ahmadiyya kwa wakati huu. Na huko India, idadi iliyopo mbele yangu ni tisini na tatu, yawezekana ofisi ya wakfe nau wamekosea tarakimu, wanapaswa kuwa zaidi, Ujerumani wako sabini, hii ni taarifa ya nyuma, kwa wakati huu yawezekana kuwa wameshaongezeka, humo wamejumuika pia watoto wa nchi mbali mbali za Ulaya, sio wa Ujerumani pekee. Jamia Ahmadiyya ya Canada wako hamsini na tano, yawezekana kwa sasa idadi hiyo ikawa imeongezeka kidogo, humo wamejumuika pia na wa Marekani. Katika Jamia Ahmadiyya ya Uingereza, kulingana na taarifa ya nyuma walikuwa ni mia moja na ishirini, pengine idadi yaweza kuwa imeshaongezeka kwa kiasi cha kumi au kumi na tano. Hapa pia wanakuja watoto toka nchi zingine za Ulaya.

Ghana wapo kumi na mbili, pengine hawa kumi na mbili ni wale wa kile chuo kipya kimechofunguliwa ambao ndio wametoa idadi yao. Hivyo hivyo Bangladesh wapo ishirini na tatu, na jumla ya idadi yote inayofahamika na ofisi husika ni elfu moja na mia nne, wakati idadi ya waakifine nau wa kiume imeshafikia karibu na elfu ishirini na nane.

Mbele yetu uwanja ni wa dunia nzima, Asia, Afrika, Ulaya, Amerika, Australia, Visiwani. Tunapaswa kufika kila mahali. Sio tu katika kila bara, au katika kila nchi, au katika kila mji, bali katika kila kitongoji na kila kijiji, twapaswa kuufikisha ujumbe mzuri wa Islam kwa kila mtu duniani. Wabashiri wachache hawawezi kuitekeleza kazi hii.

Wakati wa utotoni furaha ya kuwa ndani ya Wakfe Nau hudhihirika kidogo sana kwa watoto, lakini katika mazingira haya ya Ulaya, kutokana na mwelekeo usio sahihi wa wazazi, kwa sababu ya kuathirika na elimu ya kidunia au kwa sababu ya kukaa kwenye vijiwe vya marafiki zao, basi huelekea kwenye kusoma masomo mengine badala yale ya Jamia (ya kidini). Baadhi yao wawapo watoto husema mimi nitaenda kusoma Jamia Ahmadiyya, lakini wanapomaliza masomo ya sekondari hugeuza mwelekeo.

Bila shaka baadhi ya watoto wapo wa namna hii wenye akili sana ambao mwelekeo wao hufahamika toka utotoni, huwa na shauku isiyo ya kawaida katika baadhi ya madhumuni, kwa mfano kwenye baadhi ya madhumuni ya sayansi na kili yake inakamata vizuri huko. Hao kwa hakika wanastahili kuhamasishwa kuyasoma madhumuni hayo. Lakini wengi wao, kwa sababu tu ya kufuata mkumbo, huamua kwenda Sekondari na kuchagua baadhi ya masomo yao. Wengi wa watoto ambao nakutana nao huwauliza nao katika akili zao, hadi wamefikia darasa la kumi, huwa hawajawaza chochote kwamba wachukue masomo gani.

Hivyo kama malezi ya wazazi yatakuwa hivi tangu mwanzoni, kwamba watoe athari kwenye akili ya mtoto wao kwamba kwa vyovyote vile, mimi ni Wakfe Nau, chochote kilicho changu ni cha Jumuiya, ndipo hapo, watoto hao wataweza kufanya kazi kwa moyo sahihi na hata katika kuchagua masomo yao ya kusoma wataelekea kwenye Markaz, Jumuiya ili kupata mwongozo.

Kama nilivyosema kwamba wakati huu ni Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya tu yenye wazazi wa aina hii ambao huwatoa wakfu, kwa jadhba, watoto wao, na halafu pia huwalea kwa jadhba kwamba watoto wawe wenye kuihudumia Jumuiya na wawe wenye kustawisha roho ya wakfu. Lakini sisi hatuwezi kusema hivi kwamba wengi wa wale wanaowapeleka watoto wao kwenye Wakfe Nau kwamba wanatoa pia kipaumbele makhsus kwenye malezi yao. Hivyo wale wazazi wanaowapeleka watoto wao kwenye Wakfe Nau watatakiwa wapime kwamba zawadi hii waitoayo kwa Jumuiya wanaitendea haki kwa kiwango gani, wanajitahidi kwa kiwango gani kuirembesha zawadi hii, kwa kiwango gani wanajitahidi kuirembesha na kuikabidhi Jumuiya, ni kwa kiwango gani wanayatimiza majukumu yao.

Mkiishi katika nchi hizi zenye kila aina ya uhuru kuna umuhimu makhsus wa kuwa wazingativu sana kwenye uangalizi. Halikadhalika katika nchi masikini za Afrika na Asia msiwe msiojali baada ya kuwatoa wakfu watoto wenu, bali ni faradhi kwa wote, baba na mama, kwamba mfanye jitihada makhsus.

Pia ninawaambia watoto wa wakfe nau waliokwisha fikisha umri wa miaka kumi na mbili, kumi na tatu, kwamba waanze kujifikiria, mvitafakari vipaumbele vyenu, msitosheke na kufurahi tu kwamba sisi ni wakfe nau. Umuhimu utakuja pale utakapoyatambua makusudio yako. Je ni mwenye kuyapata? Ndipo utazalika mwelekeo wa kuelekea huko. Na wale wavulana na wasichana wenye umri wa miaka kumi na tano wanapaswa wawe na hisia zaidi ya umuhimu wao na majukumu yao.

Ndani ya aya hizi hamkuelezwa tu matashi au majukumu ya wazazi au ya nidhamu ya Jumuiya au ya kikundi fulani au ya watu fulani wachache, bali hata watoto pia wameelekezwa. Jambo la kwanza ambalo linapaswa liwepo kwa kila mtoto wa wakfe nau ni hili kwamba mama yake, kabla ya kuzaliwa kwake, aliweka tashi moyoni mwake ya kumtoa kwa ajili ya makusudio makubwa. Halafu akafanya maombi makubwa kwa unyenyekevu ya kutimiza tashi hili.

Hivyo mtoto, akiheshimu matashi na maombi ya wazazi wake, kwani wakati mwingine hata baba hushiriki katika maombi hayo, anapaswa ajitahidi kujifanya kuwa zawadi inayostahiki kwa Mwenyezi Mungu. Na hii itawezekana tu atakapouelekeza moyo wake na akili yake na kauli yake na matendo yake kulingana na ridhaa ya Mwenyezi Mungu.

Jambo la pili ni hili kwamba, kwa ajili ya wazazi wake, waliomfanyia hisani kubwa, na kutokana na kuifanya hisani hiyo, kuwe na dua hii, kwa ajili yao, kwamba upande mmoja, Mwenyezi Mungu Awarehemu, kwa upande mwingine, kila hatua waichukuayo kwa ajili ya malezi yako iwe na umuhimu moyoni mwako, na kuwe na hisia hii kwamba nami pia nishiriki katika jitihada waifanyayo wazazi wangu, kwa ajili ya kuitimiza ahadi yao, niyakubali malezi yao kwa moyo mkunjufu na nisiipoteze asilan ahadi yao.

Wakfe nau anapaswa awe ndiye mwenye haki zaidi ya kuwa na hisia ya ahadi ya kuitanguliza dini mbele ya dunia kwamba mimi ndiye napaswa kuwa wa kwanza kabisa kuitimiza na kwa kiwango cha juu kabisa.

Tatu ni kwamba, kwa ajili ya kuipata ridhaa ya Mwenyezi Mungu, ni kuweka ahadi ya kuonyesha subira na umakini katika kila aina ya kujitolea, iwe hali chungu, hali ngumu, ni lazima nitimize ahadi ya wakfu wangu katika kila sura. Tamaa yoyote ya kidunia haiwezi asilan kunitetеresha kwenye ahadi yangu ya wakfu.

Sasa kwa fadhili za Allah, kuna fadhili kubwa na hisani za Allah juu ya Jumuiya. Kuna nyakati fulani katika wa zama za Ukhalifa wa pili, katika miaka fulani huko Qadian, kulitokea hali ya aina hii kwamba kulikuwa na uhaba wa fedha kiasi hiki kwamba wafanyakazi wa Jumuiya kwa miezi mingi, ile posho waliyokuwa wamepangiwa, ilikuwa pia haiwezi kutolewa kikamilifu. Vivi hivi mwanzoni, baada ya kufanya Hijra ya kuhamia Rabwah toka Qadian, hali ya aina hii hii ilikuwepo huko Rabwah. Lakini juu ya kuwepo hali zote hizo, wale waliojitolea wakfu wa zama hizo hawakuziharibu asilan kazi zao kwa kunung'unika.

Bali haya ni mambo ya mbali, ndani ya miaka ya sabini na themanini, hali ya aina hii pia ilikuwepo katika baadhi ya nchi za Kiafrika ambapo maisha yalikuwa ni magumu sana. Ile posho iliyokuwa ikitolewa na Jumuiya ilikuwa ikimalizika ndani ya siku kumi na tano tu hadi ishirini. Wenyeji waliokuwa wamejitolea wakfu pengine waliweza kula mlo mmoja tu kwa siku, lakini daima waliienzi ahadi yao ya kujitolea wakfu na hawakulegea hata kidogo katika shughuli za mahubiri.

Jambo la nne ni hili kwamba mkuze hisia na kujitahidi kujijumuisha na watu wale wenye kueneza mema na kuzuia maovu, mtoe mfano bora wa hali ya juu sana wa khulka zenu. Mfano wa khulka za aina hiyo utakapostawi basi wema utatekelezeka, mtajiepusha na maovu. Mwelekeo wa watu wenyewe huelekea kwenye mfano mwema wa aina hiyo, watu watawaelekeeni na hivyo kupata fursa zaidi, hivyo ni muhimu sana kuihuisha hisia hiyo pamwe na kujitahidi.

Jambo la tano ni hili kwamba kwa ajili ya kuutambua wema na uovu ni kuwa na ufahamu wa Qur'an na Hadithi, kusoma vitabu na miongozo ya Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa a.s., kila wakati kujaribu kuongeza elimu ya kidini. Bila shaka yule mtoto anayesoma Jamia Ahmadiyya, huko hupatiwa elimu ya dini, lakini baada ya kumaliza hapo haifai kudhani kuwa elimu yangu sasa imefikia kikomo, bali daima ni lazima kuendelea kuiongeza elimu. Tafakkuh fid diin huwa inaleta faida wakati ambapo elimu mpya hujumuika, yanapokutana na maji mapya. Vivi hivi kwa wale ambao hawasomi jamia Ahmadiyya, nao pia wanatakiwa kudumu katika kujielimisha. Haimaanishi kwamba wale waakifine nau wasisoma Jamia Ahmadiyya wao hawana haja ya elimu ya dini. Vitabu vyovyote vipatikanavyo vinapaswa kusomwa kama vile tafsiri ya Qur'an Tukufu, na maelezo ya Qur'an Tukufu, vitabu vya Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa a.s. vilivyo katika lugha zao vinapaswa kusomwa.

Jambo la sita Ameloliagiza Mwenyezi Mungu na ambalo wakfenau wanapaswa waelekezwe ni utendaji katika uwanja wa mahubiri. Baadhi ya waakifaate nau (watoto waliotolewa wakfu wa kike) hulalamika kwamba sisi hatuna Jamia (Chuo cha Wabashiri) yaani tunakuwa hatuwezi kuipata elimu ya dini. Kama mkijisomea wenyewe, kama nilivyosema, basi mwelekeo wa kufanya mahubiri utazalika katika maeneo yao na wataipata fursa hiyo. Kwa ajili yake, mwelekeo wa mahubiri utakapozalika na fursa kupatikana basi hapo mwelekeo utakuwa ni wa kufanya maandalizi zaidi na kwa njia hii mwelekeo wa kuongeza elimu ya kidini utakuja wenyewe.

Hivyo uwanja wa mahubiri uko wazi kwa kila mtu na humo kila wakfe nau anahitajika kurukaruka na kushiriki na kila wakfe nau ajitahidi kikamilifu, anapaswa ashiriki baada ya kufikiria hivi kwamba: mimi sintotulia kabla ya kuiweka dunia chini ya bendera ya Mtume Muhammad s.a.w., na ni hisia na jadhba hii ndio itakayoelekeza pia kwenye kuongeza elimu ya dini na mwelekeo pia kuelekea kwenye mahubiri.

Jambo la saba ni kwamba kila aliyejitoa wakfu, hasa wakfe nau wanapaswa wazingatie, kwamba wao wamejumuika ndani ya kundi lile lenye jukumu la kuiokoa dunia. Kama mnayo elimu na pia mwaipata fursa, lakini kama hakuna jadhba ya kweli ya kuiokoa dunia, kama moyoni hakuna uchungu wa kumuokoa mwanadamu na maangamio, basi haitakuwepo ile jitihada ya ari inayostahili kuwepo na yawezekana kusiwemo na hata baraka.

Hivyo, kwa ajili ya kuyafikisha maneno ya Mwenyezi Mungu, kila moyo wenye uchungu pamoja na jitihada zake, unapaswa kuelekea kwenye maombi. Na ni maombi yale yenye kutokea kwenye uchungu wa moyo ndiyo, Inshaalah, yatakayotufanikisha kwenye makusudio. Hivyo kila mmoja anapaswa kukumbuka kwamba mduara wa maombi yetu usiishie kwetu tu, bali mtiririko wake uonekane kila upande ili mwanadamu yeyote asiikose

Endelea uk. 10

The First Muslim Newspaper in Kiswahili Language since 1936

MapenziyaMungu

Rabiu Thani 1434 AH | February 2013 | Tabligh 1392 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufu s.a.w

Imesimuliwa na Hadhrat Ibn Abbas r.a. ya kwamba Mjumbe wa Allah s.a.w. alisema: Hahusikani nasi yule asiyemhurumia aliye mdogo kati yetu wala asiyewaheshimu wakubwa baina yetu wala asiyeamrisha kutenda mema na kukataza maovu (*Tirmidhi*)

Mpango wa Waqfu Nau: Sifa ya pekee ya Ahmadiyya - Khalifa mtukufu

Na Mwandishi wetu

Katika hotuba ya Ijumaa ya tarehe 18 Januari 2013, Hadhrat Khalifatul Masih a.t.b.a. alizungumzia juu ya mpango wa Waqfu Nau. Alianza kwa kusoma aya ambazo tafsiri zake ni hizi:

"Wakati mwanamke fulani wa Imrani aliposema; Ee Mola wangu! Yeyote aliyemo tumboni mwangu, kwa hakika nimemtoa nadhiri Kwako nikimuepusha na misukosuko ya dunia, basi nikubalie, hakika Wewe Ndiwe Usikiae sana, Ujuaye sana.

"Basi alipofika naye katika nchi ya makimbilio, akasema: Ewe mwanangu mpendwa, kwa hakika nimeona usingizini kuwa ninakuchinja, basi tafakari na utoe rai yako. Akasema: Ewe baba yangu! Fanya kile unachoamriwa, kwa hakika, kama Allah Atapenda, basi utanikuta kuwa ni miongoni mwa wenye subira.

"Na iwepo Jumuiya moja miongoni mwenu iitayo kwenye wema na itoe mafundisho ya wema na izuie maovu na hao hao ndio watakaofaulu.

"Haiwezekani kwa waaminio kwamba wote wajitokeze, basi kwa nini isiwe hivi, kwamba katika kila madhehebu yao litokee kundi moja lipate ufahamu wa dini na kuitahadharisha kaumu yao watakaporejea kwao, ili huenda wakaokoka na maangamio."

Aya hizi ni za Sura Ali Imran, Sura Tauba na Sura Swaaffaat. Ndani ya aya hizi mmeelezwa utashi wa mama, malezi sahihi ya wazazi kwa watoto, uhamasishaji wa hisia za kujitolea za mtoto na kumuandaa, umuhimu wa kujitoa wakfu maisha na wa kazi za kujitolea wakfu na halafu makusudio ya kufanya yote haya ni yepi. Yote hayo yameelezwa ndani ya aya hizi.

Aya ya kwanza ni aya ya Sura Ali Imran, aya ya 36, humo mmedhihirishwa utashi wa mama fulani wa kumtoa wakfu mtoto kwa ajili ya dini na kuna dua ya kwamba Mungu Aukubali wakfu huo.



Hadhrat Mirza Masroor Ahmad a.t.b.a Khalifatul Masih V

Halafu ni aya ya 103 ya Sura Swaaffaat ambayo niliisoma baada ya hiyo. Humo mmetajwa malezi ya kumtayarisha baba kumtoa wakfu mwanawe kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na ya mtoto kuwa tayari kujitolea kwa kila namna kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Malezi ya baba yamemuunganisha mtoto na radhi ya Mwenyezi Mungu, na mtoto akasema: Ewe Baba! Utanikuta daima niko tayari kwa ajili ya kila namna ya kujitolea, na sio tu utanikuta niko tayari, bali utanikuta ni mwenye subira na hima ya kiwango cha juu.

Halafu nikasoma aya 105 ya Sura Ali Imran ambamo mmetajwa kundi la wenye kudumu kueneza wema na kukataza maovu. Kwani ni mambo haya haya yanayomfanya mwanadamu afanikiwe kwa njia ya ridhaa ya Mwenyezi Mungu.

Kisha mwishoni nikasoma aya ya 122 ya Sura Tauba, humo Amesema: Kuwa na ufahamu wa dini ni muhimu katika kuutambua wema na uovu. Na ufahamu wa dini ni nini? Ni sheria ya Kiislamu, ni Qur'an Karimu, kwa sababu Mwenyezi Mungu Amesema kwamba Wa radhwiitu lakumul Islaama diinan na Nimekuridhieni Islam kama dini kwa ajili yenu.

Hivyo, kwa ajili ya kuupata upendo wa Mwenyezi Mungu, ni muhimu kuifahamu Qur'an Tukufu. Na makusudio ya kufanya yote haya ni yepi? Amesema ni haya; ili ninyi muwe ni wenye kuiokoa dunia na maangamio. Hivyo haya ndiyo yale madhumuni, ambayo kwa ajili ya kuyatendea haki, Mwenyezi Mungu Ameistawisha Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya kwa njia ya Masihi Aliyeahidiwa.

Hii ndiyo ile ile Jumuiya ambayo akina mama, kabla ya kuzaliwa kwa watoto, hufanya pia maombi. Sisi tunaona tu pamwe na jadhba hii, twaona jadhba hii ikichukuliwa kwamba Rabbi inni nadhartu maa fii batwnii muharraran, fataqabbal minnii. Ee Mola Wangu, Yeyote aliyemo tumboni mwangu namtoa nadhiri Kwako nikimuepusha na misukosuko ya dunia, basi unikubalie.

Leo mfanye uchunguzi, ukiacha akina mama wa kiahmadiyya, hakuna yeyote, kwa jadhba ya aina hii, kabla ya kuzaliwa kwa mtoto, afanyaye maombi kwa Mwenyezi Mungu ya kuwatoa wakfu watoto wao. Hakuna mama yeyote leo, mbali na mama wa kiahmadiyya, tutakayempata mwenye jadhba hii. Ataonekana tu ndani ya akina mama wa kiahmadiyya, awe aishiye Pakistan au India au awe mwenye kuishi katika nchi fulani ya Asia au awe wa Afrika, awe mwenye kuishi Ulaya au wa Amerika awe mwenye kuishi Australia au huko Algeria, ambaye kwa ajili ya makusudio haya muhimu huwatoa wakfu watoto wao kwa Khalifa wa zama na halafu huwa ni wenye kuomba dua kwa Mwenyezi Mungu kwamba Ewe Allah uukubali wakfu wetu huu. Hawa wenye kuomba dua ya aina hii duniani kote hupatikana tu ndani ya akina mama wa Kiahmadiyya. Huwa wana hofu hii kwamba isije Khalifa Mtukufu akayakataa maombi yetu haya. Na sura hii na jadhba hii haiwezi kuzalika kwingine kokote, kwa sababu ni hii hii Jumuiya iliyopo chini ya kivuli cha Ukhalifa ambayo Mwenyezi Mungu Ameistawisha kwa njia ya mpenzi wa kweli wa Mtume s.a.w., yaani Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa a.s.

Halafu haikuishia hapo, ni ndani ya Jumuiya hii hii ya Ahmadiyya waliomo wale akina baba ambao huwalea tu watoto wao kwamba afikapo umri wa ujana awe tayari kwa ajili ya kila aina ya kujitolea na (kijana huyo) humuandikia Khalifa wa zama kwamba ahadi ya kwanza ni ya wazazi wangu na ahadi ya pili ni yangu. Sasa unipeleke popote utakapo kwa ajili ya kujitolea. Sasa daima utanikuta mimi kuwa ni mwenye subira na mwenye kuonyesha istiqama na hutanikuta kuwa ni mwenye kurudi nyuma kwa ahadi waliyoiweka wazazi wangu.

Hao ndio wale watoto wanaoitwa kuwa ni wenye uaminifu kwa umati wa Muhammad. Hao ndio wale watu wenye kutoa haki ya kuwemo ndani ya umati wa Mtume Muhammad s.a.w. Malezi ya wazazi na asili ya wema ya mtoto iliwafundisha namna ya kutoa haki ya Allah na pia kuwafundisha kiwango cha utoaji wa haki za viumbe wa Allah, waliopata pia

Endelea uk. 11

Madaktari Uingereza watoa risasi iliyopigwa puani

Na Pazi Kitabu Mazongera.

Madaktari wa Hospitali ya Queen Elizabeth nchini Uingereza wamefanikiwa kutoa risasi iliyopigwa puani na kumfanya kurejesha uwezo wake wa kuona kijana wa Ahmadiyya mwenye umri wa miaka 22 raia wa Pakistan.

Kijana huyo ambaye alikuwa anasoma Chuo Kikuu cha Sunderland masuala ya fedha alipigwa risasi kwenye tukio la ndoa ya ndugu yake Saad, alikuwa anaona vitu viwili viwili na wakati mwingine kushindwa kuona vizuri

Daktari bingwa kiongozi wa masiko, puana koo Dr. Shahzada Ahmed alifanikiwa kutoa risasi hizo kutoka kijana huyo aitwaye Ummad Farooq kwa kutumia teknolojia ya kisasa kwa kifaa kiitwacho Cyclops. Kifaa hicho kinamwezesha daktari kufaa upasuaji kwa haraka na ufanisi zaidi bila ya madhara kwa mgonjwa. Upasuaji huo ulichukua saa moja na kurudisha uwezo wa kuona wa kijana huyo.

Farooq akiwashukuru madaktari waliomfanyia upasuaji huo alisema, "madaktari nchini Pakistani waliniambia upasuaji huo ni wa hatari kwake na ungeweza kumfanya awe kipofu" na hivyo kumfanya aende Uingereza kwa matibabu zaidi. Nilipofika Uingereza bado



Ummad Farooq baada ya kufanyiwa upasuaji

risasi ilizidi kujichimbia kwa ndani ya mishipa ya jicho na kunifanya nione vitu vikiwa viwili viwili. Baada ya upasuaji huo sasa naona kama kawaida.

Aliliambia gazeti la Daily Mail la nchini Uingereza.

Akieleza sakata hilo alisema alikwenda Karachi kwenye ndoa ya kaka yake iliyofanyika tarehe 19 Octoba mwaka jana na kutokea vurugu iliyoanzishwa na baadhi ya wanandugu ambapo bwana harusi Saad alifariki na baba yake alipigwa risasi tano na bado ziko mwilini hadi sasa na hali yake ni nzuri. Alisema.

Alisema baba yake ni Rais wa Jamaat ya Ahmadiyya Karachi na kwa sababu za kitofauti za kiimani baadhi ya watu walitumia nafasi hiyo kufanya mauaji hayo na kutujeruhi, kabla hatujahamishiwa kwenye nyumba nyingine kwa usalama wetu. Jumuiya yangu ya Ahmadiyya Karachi imeamua kunipeleka kwa matibabu zaidi nje ya nchi.

Daktari alisema kuwa hajawahi kutumia teknolojia hiyo kwa kutoa risasi hizo kupitia pua na hivyo kuwa ni upasuaji wa kipekee kwa kuleta mafanikio. Alimalizia daktari Ahmed.

Huo ni muendelezo wa mauaji na mateso wanayopata Waislamu wa Jumuiya ya Ahmadiyya nchini Pakistan na kwingineko duniani. Tunaamini mateso haya ni katika sunna ambazo Waislamu wengine wamezikosa na kuthibitisha ukweli wa madai yetu. Mwenyezi Mungu amlaze pema peponi Saad. Amin. Innalillah Wainnaillah Raj'uun.